

القرآن الحكيم

QURANI TAKATIFU

Swahili Quran Translation

by

Sheikh Abdullah Saleh Al-Farsy
(Former Chief Kadhi of
Zanzibar & Kenya)

32. Basi ni nani dhalimu mkubwa kuliko yule anayemsingizia uwongo Mwenyezi Mungu na kuikadhibisha kweli imjiapo? Je, siyo katika Jahanamu makazi ya hao makafiri?

33. Na aliyeleta ukweli na aliyeusadikisha — hao ndio wamchao Mwenyezi Mungu.

34. Watapata watakachotaka kwa Mola wao; hayo ndiyo malipo ya watendao mema;

35. Ili Mwenyezi Mungu awafutie ubaya walioufanya na kuwalipa ujira wao kwa wema waliokuwa wakiutenda.

36. Je, Mwenyezi Mungu hamkifii (hamtoshei), mja wake? Na wanakuogofisha (wanakukhofisha) wale walio kinyume chake, (masanamu; kuwa watakudhuru kama hutawaabudu. Wanaweza wapi kudhuru, licha kunufaisha!). Na aliyehukumiwa na Mwenyezi Mungu kupotea, basi hana wa kumuongoa.

37. Na ambaye Mwenyezi Mungu anamuongoa hakuna awezaye kumpoteza, Je! Mwenyezi Mungu si Mwenye nguvu, anayeweza kulipa kisasi?

38. Na ukiwauliza: “Ni nani aliyeziumba mbingu na ardhi?” Bila shaka watasema: “Ni Mwenyezi Mungu.” Sema: “Je, Mnawaonaje wale mnaowaomba kinyume cha Mwenyezi Mungu, kama Mwenyezi Mungu akitaka kunidhuru, wao wanaweza kuniondolea dhara yake? au akitaka kunirehemu, je, wao wanaweza kuzuia rehema yake?” Sema: “Mwenyezi Mungu ananitoshia, kwake wategemea wanaotegemea ”

39. Sema: “Enyi watu wangu! Fanyeni amali zenu kwa tamkini yenu, (mpendavyo), mimi pia nafanya (kwa tamkini yangu). Basi karibuni hivi mtajua ”

40. “Ni nani itakayemjia adhabu ya kumfedhehesha na itakayemshukia adhabu iendeleayo.”

41. Sisi tumekuteremshia Kitabu hiki kwa ajili ya watu (wote) ili kuwabainishia haki, basi anayeongoka (anaongoka) kwa manufaa ya nafsi yake, na anayepotoka bila shaka anapotoka kwa hasara (ya nafsi) yake pia. Na wewe siye mlinzi wao.

فَمَنْ أَظْلَمُ مِمَّنْ كَذَبَ عَلَى اللَّهِ وَكَذَّبَ بِالصِّدْقِ إِذْ جَاءَهُ ۗ أَلَيْسَ فِي جَهَنَّمَ مَثْوًى لِّلْكَافِرِينَ ﴿٣٢﴾
وَالَّذِي جَاءَ بِالصِّدْقِ وَصَدَّقَ بِهِ ۖ أُولَٰئِكَ هُمُ الْمُتَّقُونَ ﴿٣٣﴾

لَهُمْ مَا يَشَاءُونَ عِندَ رَبِّهِمْ ۚ ذَٰلِكَ جَزَاؤُ الْمُحْسِنِينَ ﴿٣٤﴾
يُكَفِّرُ اللَّهُ عَنْهُمْ أَسْوَأَ الَّذِي عَمِلُوا وَيَجْزِيهِمْ أَجْرَهُمْ بِأَحْسَنِ الَّذِي كَانُوا يَعْمَلُونَ ﴿٣٥﴾
أَلَيْسَ اللَّهُ بِكَافٍ عَبْدَهُ ۗ وَيُخَوِّفُونَكَ بِالَّذِينَ مِنْ دُونِهِ ۗ وَمَنْ يُضِلِلِ اللَّهُ فَمَا لَهُ مِنْ هَادٍ ﴿٣٦﴾

وَمَنْ يَهْدِ اللَّهُ فَمَا لَهُ مِنْ مُضِلٍّ ۗ أَلَيْسَ اللَّهُ بِعَزِيزٍ ذِي انْتِقَامٍ ﴿٣٧﴾

وَلَيْنَ سَأَلْتَهُمْ مَنْ خَلَقَ السَّمَوَاتِ وَالْأَرْضَ لَيَقُولُنَّ
اللَّهُ ۗ قُلْ أَفَرَأَيْتُمْ مَا تَدْعُونَ مِنْ دُونِ اللَّهِ إِنْ أَرَادَنِيَ اللَّهُ بِضُرٍّ هَلْ هُنَّ كَافٍتٌ صُورُهُ أَوْ أَرَادَنِي بِرَحْمَةٍ هَلْ هُنَّ مُمْسِكَتٌ رَحْمَتُهُ ۗ قُلْ حَسْبِيَ اللَّهُ عَلَيْهِ يَتَوَكَّلُ الْمُتَوَكِّلُونَ ﴿٣٨﴾

قُلْ يَقَوْمِ اعْمَلُوا عَلَىٰ مَكَانَتِكُمْ إِنِّي عَامِلٌ ۗ سَوْفَ تَعْمَلُونَ ﴿٣٩﴾

مَنْ يَأْتِيهِ عَذَابٌ يُخْزِيهِ وَيَحِلُّ عَلَيْهِ عَذَابٌ مُّقِيمٌ ﴿٤٠﴾

إِنَّا أَنْزَلْنَا عَلَيْكَ الْكِتَابَ لِلنَّاسِ بِالْحَقِّ ۗ فَمَنْ اهْتَدَىٰ فَلِنَفْسِهِ ۖ وَمَنْ ضَلَّ فَإِنَّمَا يَضِلُّ عَلَيْهَا ۗ وَمَا أَنْتَ بِمُكَيِّدٍ ﴿٤١﴾

36. Nawasikie wanaoomba makaburi na mizimu na . . . wakamuacha Mwenyezi Mungu. Mwenyezi Mungu hawezi kuwatosheliza? Na waisome vile vile Aya ya 38 na ya 43 na ya 44 na ya 45 za Sura hii hii. Wanataka waambiweje zaidi kuliko hivi?

42. Mwenyezi Mungu hutakabadhi roho wakati wa mauti yao. Na zile (roho) zisizokufa (bado, pia Mwenyezi Mungu anazitakabadhi) katika usingizi wao. Basi huzizuia zile alizozikidhia mauti, (alizozi hukumia kufa), na huzirudisha zile nyingine mpaka (ufike) wakati uliowekwa. Bila shaka katika hayo yamo mazingatio kwa watu wanaotafakari.

43. Au ndio wamejifanyia waombezi mbele ya Mwenyezi Mungu? Sema: "Ingawa hawana mamlaka juu ya kitu chochote, wala hawatambui lolote?"

44. Sema: "Uombezi wote uko katika amri ya Mwenyezi Mungu; ambaye ndiye mwenye ufalme wa mbingu na ardhi, kisha mtarejeshwa kwake."

45. Na anapotajwa Mwenyezi Mungu peke yake nyoyo za wale wasioamini Akhera huchukiwa. Na wanapotajwa wale walio kinyume naye, mara wanafurahi.

46. Sema: "Ee Mola! Muumba wa mbingu na ardhi, Mjuzi wa yasiyoonekana na yanayoonekana. Wewe utahukumu baina ya waja wako katika yale waliyokuwa wakihitalifiana. (Basi tuongoe njia ya haki si njia za hao waliopotea)."

47. Na kama madhalimu wanalikuwa na vyote vinavyopatikana katika ardhi, na pamoja navyo vingine kama hivyo, bila shaka wanalivitoa kujikomboa katika adhabu mbaya siku ya Kiama. Na yatawadhihirikia kwa Mwenyezi Mungu ambayo hawakuwa wakiyatazamia, (wakiyadhani).

48. Na utawadhihirikia ubaya wa yale waliyoyachuma, na yatawazunguka yale waliyokuwa wakiyafanyia mzaha.

49. Na dhara inapomgusa mwanadamu hutuomba; kisha tunapompa neema zitokazo kwetu, husema: "Nimepewa (neema hizo) kwa sababu ya ujuzi wangu; (kwa hivyo sina haja ya kumshukuru Mwenyezi Mungu);" Siyo! huo ni mtihani (tu anafanyiwa) lakini wengi wao hawajui (kitu).

50. Waliyasema haya wale waliokuwa kabla yao, lakini hayakuwafaa waliyokuwa wakiyachuma.

اللَّهُ يَتَوَكَّلُ عَلَى الْإِنْسَانِ حِينَ مَوْتِهَا وَ الَّتِي أَمَرْتُمْ فِي مَنَامِهَا: قِيمُكَ الَّتِي قَضَى عَلَيْهَا أَمُوتَ وَيُرْسِلُ الْأُخْرَى إِلَى أَجَلٍ مُّسَمًّى إِنَّ فِي ذَلِكَ لَآيَاتٍ لِّقَوْمٍ يَتَفَكَّرُونَ ﴿٤٢﴾

أَمْرًا تَخْذُوا مِنْ دُونِ اللَّهِ شِعْقَاءً قُلْ أُولَئِكَ لَا يَعْلَمُونَ شَيْئًا وَلَا يَعْهَدُونَ ﴿٤٣﴾

قُلْ لِلَّهِ الشَّفَاعَةُ جَمِيعًا لَهُ مُلْكُ السَّمَوَاتِ وَالْأَرْضِ ثُمَّ إِلَيْهِ تُرْجَعُونَ ﴿٤٤﴾

وَإِذَا ذُكِرَ اللَّهُ وَحْدَهُ اشْتَرَّتْ قُلُوبُ الَّذِينَ لَا يُؤْمِنُونَ بِالْآخِرَةِ: وَإِذَا ذُكِرَ الَّذِينَ مِنْ دُونِهِ إِذَا هُمْ يَسْتَبْشِرُونَ ﴿٤٥﴾

قُلِ اللَّهُمَّ فَاطِرَ السَّمَوَاتِ وَالْأَرْضِ عَلِيمَ الْغَيْبِ وَالشَّهَادَةِ أَنْتَ تَحْكُمُ بَيْنَ عِبَادِكَ فِي مَا كَانُوا فِيهِ يَخْتَلِفُونَ ﴿٤٦﴾

وَلَوْ أَنَّ لِلَّذِينَ ظَلَمُوا مَا فِي الْأَرْضِ جَمِيعًا وَمِثْلَهُ مَعَهُ لَا فُتِنُوا بِهِ مِنْ سُوءِ الْعَذَابِ يَوْمَ الْقِيَامَةِ: وَبَا أَلْهُمَّ مَنْ اللَّهُ مَا لَمْ يَكُونُوا يَحْتَسِبُونَ ﴿٤٧﴾

وَبَا أَلْهُمَّ سَيِّئَاتُ مَا كَسَبُوا وَحَاقَ بِهِمْ مَا كَانُوا بِهِ يَسْتَهْزِئُونَ ﴿٤٨﴾

فَإِذَا مَسَّ الْإِنْسَانَ صُدُورُهُ قَالَ وَإِذْ أَوْحَيْنَا إِلَيْهِ نَعْمَةً مِنَّا: قَالَ إِنَّمَا أَوْحَيْتُنِي عَلَىٰ عِلْمٍ بَلَّغِي فَتَنَةٌ وَلَكِنَّكُمْ أَكْثَرُهُمْ لَا يَعْلَمُونَ ﴿٤٩﴾

قَدْ قَالُوا الَّذِينَ مِنْ قَبْلِهِمْ فَمَا أَخْنَىٰ عَنْهُمْ مَا كَانُوا يَكْسِبُونَ ﴿٥٠﴾

42. Makadiyani wamesema uwongo katika tamko la *Yatawaffaa* lililoko katika hii Aya waliyoifanya ni ya 43. Turnebainisha uwongo wao huu katika marejezo ya Aya ya 55 ya *Surat Aali Imran*, na katika Aya ya 117 ya *Suratul Maida* na katika Aya ya 60 ya *Suratul An-Am* vile vile.

51. Basi ukawasibu ubaya wa yale waliyoyachuma. Na wale waliodhulumu miongoni mwa hawa, karibuni nao utawasibu ubaya wa yale waliyoyachuma. Nao si wenye kumshinda (Mwenyezi Mungu).

52. Je! Wao hawajui ya kwamba Mwenyezi Mungu hutoa riziki (nyingi) kwa yule amtakaye na akamdhikishia (amtakaye)? Kwa hakika katika hayo yako mazingatio kwa watu wanaoamini.

53. Sema, “Enyi waja wangu mliojidhulumu nafsi zenu! Msikate tamaa na rehema ya Mwenyezi Mungu; bila shaka Mwenyezi Mungu husamehe dhambi zote; hakika yeye ni Mwingi wa kusamehe (na) Mwingi wa kurehemu.”

54. “Na rejeeni kwa Mola wenu na mnyenyekee kwake kabla ya kukujieni adhabu, kisha hamtanusuriwa.”

55. “Na fuateni yaliyo bora katika yale yaliyoteremshwa kwenu kutoka kwa Mola wenu kabla ya kukujieni adhabu kwa ghafla, na hali hamtambui

56. “Isije ikasema nafsi (asiye akasema mtu): ‘ Eee majuto yangu kwa yale niliyopunguza upande wa Mwenyezi Mungu, na hakika nilikuwa miongoni mwa wanaoyafanyia mzaha (mambo ya dini) ”

فَأَصَابَهُمْ سَيِّئَاتُ مَا كَسَبُوا. وَالَّذِينَ ظَلَمُوا مِنْ هَؤُلَاءِ سَبَّيْنَهُمْ سَيِّئَاتُ مَا كَسَبُوا. وَمَأْتِهِمْ مُجْرِمِينَ ﴿٥١﴾

أَوَلَمْ يَعْلَمُوا أَنَّ اللَّهَ يَبْسُطُ الرِّزْقَ لِمَنْ يَشَاءُ وَيَقْدِرُ. إِنَّ فِي ذَلِكَ لَآيَاتٍ لِقَوْمٍ يُؤْمِنُونَ ﴿٥٢﴾

قُلْ يِعَادِي الَّذِينَ ظَلَمُوا أَنفُسِهِمْ لَا تَقْنَطُوا مِنْ رَحْمَةِ اللَّهِ إِنَّ اللَّهَ يَغْفِرُ الذُّنُوبَ جَمِيعًا إِنَّهُ هُوَ الْغَفُورُ الرَّحِيمُ ﴿٥٣﴾

وَأَنبِئُوا إِلَىٰ رَبِّكُمْ وَأَسْلُمُوا لَهُ مِنْ قَبْلِ أَنْ يَأْتِيَكُمُ الْعَذَابُ ثُمَّ لَا تُنصَرُونَ ﴿٥٤﴾

وَأَتَّبِعُوا أَحْسَنَ مَا أُنزِلَ إِلَيْكُمْ مِنْ رَبِّكُمْ وَمِنْ قَبْلِ أَنْ يَأْتِيَكُمُ الْعَذَابُ بَغْتَةً وَأَنْتُمْ لَا تَشْعُرُونَ ﴿٥٥﴾

أَنْ تَقُولَ نَفْسٌ يَحْسَبُنِي عَلَىٰ مَا فَكَّرْتُ فِي حَيْبِ اللَّهِ وَإِن كُنْتُ لَمِنَ السَّخِرِينَ ﴿٥٦﴾

53. *Alhamdu Lillah.* Mwenyezi Mungu anatupa bishara isiyokuwa na mfano. Hapana katika Qurani nzima Aya ya kutumainisha zaidi kuliko Aya hii. Basi naturejee kwa Mwenyezi Mungu upesi kama alivyotwambia katika Aya zinazofuatia hapa mpaka ya 61.

Na kurejea kwa makosa yaliyo baina yako na Mola wako ni (a) Kuacha makosa hayo; (b) Kujuta ukaona vibaya kuwa uliyafanya; (c) Kuazimia kweli kweli kutoyafanya tena; na (d) Kulipa kinachoweza kulipika, kama Sala na Saumu.

Na yakiwa makosa haya yameshikamana na haki za watu. Basi yakiwa mali, upesi uwarejeshee wenyewe kwa njia yoyote ile, ikiwa ya dhahiri au ya siri — isiyokuwa na khatari nawe. Lakini kila namna upesi warejeshewe. Wakiwa hawapo werejeshée warithi wake, wagawe wenyewe au — kama hawajui — uwagawie wewe.

Ikiwa uliyowakosa ni kuwavunjia hishima zao, basi kawatake msamaha kwa unyenyekevu wakusamehe. Likiwa jambo hilo halimkiniki kuwaambia, basi watolee masadaka ili wapewe siku ya Kiama thawabu za sadaka hizo ili wakusamehe wakiona wamekwisha kupata badala yake.

Basi Mwenyezi Mungu ni wa kushukuriwa. *Al Hamdulillah*

Alhamdu Lillahi	Mola wetu Subhana
Mola asiye shabihi	Na mfano wake hana
Ametukuka Ilahi	Hana mke hana mwana
Mwengine hana maana	Haqadimu haakhiri
Hamdi ninahimidi	Namshukuru Wadudi
Shukuru isiyo hadi	Kwa zote zake neema
Alhamdu Lillahi	Yeye pweke ni Ilahi
Jioni na asubuhi	Namshukuru Karima
Amenivika Samadi	Neema zisizo hadi
Mimi ninazifaidi	Na wenzangu kwa daima

Ninashukuru hivi na zaidi kwa ajili ya maamrisha ya Aya ya 66 iliyoko hapa na nyingi nyingine mno kabisa zilizojaa katika Qurani na Hadithi za Mtume.

57. Au ikasema: “Kama Mwenyezi Mungu angeniongoa, bila shaka ningekuwa miongoni mwa wenye kumcha Mwenyezi Mungu”

58. Au ikasema ionapo adhabu: “Kama ningepata marejeo (ya kurejea tena duniani) ningekuwa miongoni mwa wafanyao mema.”

59. (Ataambiwa): “Kwa nini! Bila shaka zilikuja Aya zangu ukazikadhibisha na ukajivuna na ukawa miongoni mwa makafiri.”

60. Na siku ya Kiama utawaona wale waliomsingizia uwongo Mwenyezi Mungu nyuso zao zimekuwa nyeusi. Je, si katika Jahanamu makazi ya wale wanaotakabari?

61. Na Mwenyezi Mungu atawaokoa wale wamchao kwa ajili ya kufuzu kwao, (mafanikio yao). Hautawagusa ubaya wala hawatahuzunika.

62. Mwenyezi Mungu ndiye Muumba wa kila kitu na yeye ndiye Mlinzi juu ya kila kitu.

63. Funguo za mbingu na ardhi ziko kwake, na wale waliozikanusha Aya za Mwenyezi Mungu hao ndio wenye hasara.

64. Sema: “Je! Mnaniamrisha niabudu asiyekuwa Mwenyezi Mungu enyi wajinga!”

65. Na kwa yakini yamefunuliwa kwako na kwa wale waliokuwa kabla yako (maneno haya):- “Kama ukimshirikisha (Mwenyezi Mungu) bila shaka amali zako zitaruka patupu, (hutazipatia thawabu japo ni amali njema); na lazima utakuwa miongoni mwa wenye hasara.”

66. Bali muabudu Mwenyezi Mungu tu na uwe miongoni mwa wenye kushukuru.

67. Na hawakumhishimu Mwenyezi Mungu hishima ipasayo. Na siku ya Kiama ardhi yote itakuwa mkononi Mwake, na mbingu zitakunjwa katika mkono Wake wa kuume, (kulia). Ameepukana na upungufu na yu juu kabisa kuliko yale wanayomshirikishiya.

68. Na litapigwa baragumu watoke roho watu waliomo mbinguni na waliomo ardhini ila yule amtakaye Mwenyezi Mungu. Tena litapigwa mara nyingine. Hapo watafufuka (wote); wawe wanatazama (nini litatokea).

أَوْ تَقُولَ لَوْ أَنَّ اللَّهَ هَدَانِي لَكُنْتُ مِنَ الْمُتَّقِينَ ﴿٥٧﴾

أَوْ تَقُولَ لَئِن تَرَى الْعَذَابَ لَأُوتِيَ كَرْهًا فَاكُونُ مِنَ الْخَائِبِينَ ﴿٥٨﴾

بَلْ قَدْ جَاءَكَ آيَاتِي فَكَدَّبْتَ بِهَا وَاسْتَكْبَرْتَ وَكُنْتَ مِنَ الْكٰفِرِينَ ﴿٥٩﴾

وَيَوْمَ الْقِيَامَةِ تَرَى الَّذِينَ كَذَبُوا عَلَى اللَّهِ وُجُوهُهُم مُّسْوَدَّةٌ أَلَيْسَ فِي جَهَنَّمَ مَثْوًى لِّلْمُتَكَبِّرِينَ ﴿٦٠﴾

وَيُنَادِي اللَّهُ الَّذِينَ اتَّخَفُوا عَفَا ذَنبِهِمْ وَلَا يَسْمَعُ السُّوءَ وَلَا هُمْ يَحْزَنُونَ ﴿٦١﴾

اللَّهُ خَالِقُ كُلِّ شَيْءٍ وَهُوَ عَلَىٰ كُلِّ شَيْءٍ وَكِيلٌ ﴿٦٢﴾

لَهُ مَقَالِيدُ السَّمٰوٰتِ وَالْاَرْضِ وَالَّذِينَ كَفَرُوا بِآيٰتِ اللَّهِ اُولٰٓئِكَ هُمُ الْخٰسِرُونَ ﴿٦٣﴾

قُلْ اَفَغَيْرَ اللَّهِ تَمْرُوْنَ اَعْبُدُ اَيُّهَا الْجٰهِلُونَ ﴿٦٤﴾

وَلَقَدْ اَوْحٰى اِلَيْكَ وَاِلَى الَّذِيْنَ مِنْ قَبْلِكَ: لَنْ اَشْرَكَتْ لِيَحْبَطَ عَنْكَ عَمَلُكَ وَلَنْ تَكُوْنَنَّ مِنَ الْخٰسِرِيْنَ ﴿٦٥﴾

بَلِ اللّٰهُ فَاعْبُدْ وَكُنْ مِنَ الشّٰكِرِيْنَ ﴿٦٦﴾

وَمَا قَدَرُوا اللّٰهَ حَتّٰى قَدَرَهُ ۗ وَالْاَرْضُ جَبِيْنًا قَبْضَتُهٗ يَوْمَ الْقِيٰمَةِ وَالسَّمٰوٰتُ مَطْوِيٰتٌ بِيَمِيْنِهٖ ۗ سُبْحٰنَهٗ وَتَعَالٰى عَمَّا يُشْرِكُوْنَ ﴿٦٧﴾

وَنُفِخَ فِي الصُّوْرِ فَصَعِقَ مَنْ فِي السَّمٰوٰتِ وَمَنْ فِي الْاَرْضِ اِلَّا مَنْ شَاءَ اللّٰهُ ثُمَّ نُفِخَ فِيْهِ اٰخَرَ مَرَّةٍ فَاِذَا هُمْ قِيٰمٌ يَنْظُرُوْنَ ﴿٦٨﴾

69. Na ardhi (siku hiyo) itang'ara kwa nuru ya Mola wake, na madaftari (ya vitendo) yatawekwa; na wataletwa Manabii na mashahidi, na kutahukumiwa baina yao kwa haki wala hawatadhulumiwa.

70. Na kila nafsi italipwa kwa yale iliyoyafanya, naye (Mwenyezi Mungu) anajua sana wanayoyatenda.

71. Na waliokufuru watapelekwa katika Jahanamu makundi-makundi; mpaka watakapoifikia itafunguliwa milango yake; na walinzi wake watawaambia: "Je! hawakukujieni Mitume miongoni mwenu wakikusomeeni Aya za Mola wenu na kukuonyeni makutano ya siku yenu hii?" Watasema: "Kwa nini? (Wametujia)! Lakini limethubuti neno la adhabu juu ya wale waliowakanusha. (Nao ndio sisi)."

72. Itasemwa: "Ingieni milango ya Jahanamu mkakae humo." Basi ni ubaya ulioje wa makazi ya wanaotakabari!

73. Na waliomcha Mola wao watapelekwa Peponi makundi makundi; mpaka watakapoifikia (wataingia tu na wataikuta) milango yake imekwishafunguliwa; na walinzi wake watawaambia: "Amani juu yenu, furahini, ingieni humu mkae milele."

74. Nao watasema: "Sifa zote njema ni za Mwenyezi Mungu ambaye ametutimizia ahadi yake na ameturithisha ardhi (ya huku Peponi); tunakaa katika Mabustani haya popote tupendapo." Basi ni malipo mazuri yaliyoje ya watendao (mema)!

75. Na utawaona Malaika wakizunguka pembeni mwa Kiti cha enzi (cha Mwenyezi Mungu), wakimtukuza na kumsifu Mola wao. Na kutahukumiwa baina yao kwa haki na kutasemwa: "Sifa zote njema ni za Mwenyezi Mungu, Mola wa viumbe vyote."

وَأَشْرَقَتِ الْأَرْضُ بِنُورِ رَبِّهَا وَوُضِعَ الْكِتَابُ
وَجَاءَ رَبُّنَا بِالْبَيِّنَاتِ وَالشَّهَادَةِ وَقُضِيَ بَيْنَهُم بِالْحَقِّ
وَهُمْ لَا يُظْلَمُونَ ﴿٦٩﴾

وَوُفِّيَتْ كُلُّ نَفْسٍ مَّا عَمِلَتْ وَهُوَ أَعْلَمُ بِمَا
يَفْعَلُونَ ﴿٧٠﴾

وَسَيَقُ الِّذِينَ كَفَرُوا إِلَىٰ جَهَنَّمَ زُمَرًا حَتَّىٰ إِذَا
جَاءَهَا فَفُتِحَتْ أَبْوَابُهَا وَقَالَ لَهُمْ خَزَنَتُهَا أَلَمْ
يَأْتِكُمْ رُسُلٌ مِّنكُمْ يَتْلُونَ عَلَيْكُمْ آيَاتِ رَبِّكُمُ
وَيُنذِرُونَكُمْ لِقَاءَ يَوْمِكُمْ هَٰذَا قَالُوا بَلَىٰ وَلَكِن
حَقَّتْ كَلِمَةُ الْعَذَابِ عَلَى الْكَافِرِينَ ﴿٧١﴾


فَيَلِدُ اُدْخُلُوا أَبْوَابَ جَهَنَّمَ خَالِدِينَ فِيهَا فَبِئْسَ
مَثْوَى الْمُتَكَبِّرِينَ ﴿٧٢﴾

وَسَيَقُ الِّذِينَ اتَّقَوْا رَبَّهُمْ إِلَىٰ الْجَنَّةِ زُمَرًا
حَتَّىٰ إِذَا جَاءَهَا فَفُتِحَتْ أَبْوَابُهَا وَقَالَ لَهُمْ خَزَنَتُهَا
سَلَامٌ عَلَيْكُمْ طِبْتُمْ فَادْخُلُوهَا خَالِدِينَ ﴿٧٣﴾

وَقَالُوا الْحَمْدُ لِلَّهِ الَّذِي صَدَقَنَا وَعْدَهُ وَأَوْرَثَنَا
الْأَرْضَ نَتَّبِعُونَ آيَاتِهِ مِنَ الْجَنَّةِ حَيْثُ نَشَاءُ فَنِعْمَ أَجْرُ
الْعَامِلِينَ ﴿٧٤﴾

وَتَرَى الْمَلَائِكَةَ حَافِينَ مِنْ حَوْلِ الْعَرْشِ
يُسَبِّحُونَ بِحَمْدِ رَبِّهِمْ وَقُضِيَ بَيْنَهُم بِالْحَقِّ
رَبُّ الْعَالَمِينَ ﴿٧٥﴾

71. Basi natutengenee kabla ya kusimangwa kwa Aya hii na nyinginezo. Aliyeonya, Hana Lawama Akitesa. Na Mwenyezi Mungu ametuonya kweli kweli.



Ina Aya 85

SURATUL MUUMIN
(Imeteremka Makka)

Ina Makara 9

Kwa jina la Mwenyezi Mungu, Mwenye kuneemesha neema kubwa kubwa, na Mwenye kuneemesha neema ndogo ndogo.

بِسْمِ اللَّهِ الرَّحْمَنِ الرَّحِيمِ

1. Haa Mym.

حَمْدٌ

2. Kuteremshwa kwa Kitabu (hiki) kunatokana kwa Mwenyezi Mungu, Mwenye nguvu, Mwenye kujua

تَنْزِيلُ الْكِتَابِ مِنَ اللَّهِ الْعَزِيزِ الْعَلِيمِ

3. Anayeghufiria dhambi na anayepokea toba, Mkali wa kuadhibu, Mwenye ukarimu; hakuna aabudiwaye kwa haki ila yeye; (na) marejeo ni kwake.

غَافِرِ الذَّنْبِ وَقَابِلِ التَّوْبِ شَدِيدِ الْعِقَابِ ذُكَّرَ الطَّوْلِ وَالْأَمَالِ إِلَّا هُوَ إِلَهُ الْمَصِيرِ

4. Hawabishi katika Aya za Mwenyezi Mungu ila wale waliokufuru; basi kusikudanganye kutembeatembea kwenye katika nchi. (Mara moja tutawatia mkononi).

مَا يُجَادِلُ فِي آيَاتِ اللَّهِ إِلَّا الَّذِينَ كَفَرُوا فَلَا يَغْرُرْكَ تَقَلُّبُهُمْ فِي الْبِلَادِ

5. Watu wa Nuhu walikadhibisha kabla yao (hawa watu wako); na makundi (mengine) baada yao (yalikadhibisha pia), na kila taifa liliazimia baya juu ya Mtume wao ili wamkamate (wamuue); na walibishana kwa ubatili ili kuipindua haki. Kwa hivyo niliwatia mkononi (niliwakamata). Basi likuwaje adhabu yangu!

كَذَّبَتْ قَبْلَهُمْ قَوْمُ نُوحٍ وَالْأَحْزَابُ مِنْ بَعْدِهِمْ وَهَمَّتْ كُلُّ أُمَّةٍ بِرَسُولِهِمْ لِيَأْخُذُوهُ وَجَادَلُوا بِالْبَاطِلِ لِيُدْحِضُوا بِهِ الْحَقَّ فَأَخَذْتُهُمْ فَكَيْفَ كَانَ عِقَابِ

6. Namna hivi limewathubutikia makafiri neno la Mola wako ya kwamba wao ni watu wa Motoni.

وَكَذَلِكَ حَقَّتْ كَلِمَتُ رَبِّكَ عَلَى الَّذِينَ كَفَرُوا إِنَّهُمْ أَصْحَابُ النَّارِ

7. Wale wanaokichukua Kiti cha Enzi (cha Mwenyezi Mungu) na wale wanaokizunguka, wanamtukuza Mola wao na kumsifu na wanamuamini na wanawaomba samahani walioamini, (wanasema): "Mola wetu! Umekienea kila kitu kwa rehema na ilimu (Unakijua kila kitu). Basi wasamehe waliotubu na wakaifuata njia yako na waepushe na adhabu ya Jahanamu."

الَّذِينَ يَحْمِلُونَ الْعَرْشَ وَمَنْ حَوْلَهُ يُسَبِّحُونَ بِحَمْدِ رَبِّهِمْ وَيُؤْمِنُونَ بِهِ وَيَسْتَغْفِرُونَ لِلَّذِينَ آمَنُوا رَبَّنَا وَسِعْتَ كُلَّ شَيْءٍ رَحْمَةً وَعِلْمًا فَاغْفِرْ لِلَّذِينَ تَابُوا وَاتَّبَعُوا سَبِيلَكَ وَقِهِمْ عَذَابَ الْحَجِيمِ

وَالَّذِينَ آمَنُوا وَعَمِلُوا الصَّالِحَاتِ لَهُمْ أَجْرٌ كَثِيرٌ

3. Mwenyezi Mungu ana sifa zote hizi mbili. Basi tusighurike kwa ile moja tu ya Rehema. "Ukibebwa Usiregee" na "Ukipakatwa Usipwetekee." Usimvunje nguvu — wala moyo — anayekusaidia, atakuchukua.

7. Unaona hapa Malaika wanawaomba msamaha wale WANAOREJEA kwa Mwenyezi Mungu, si kila

8. “Mola wetu! Waingize katika Mabustani ya milele uliyowaahidi. Na uwape haya pia waliofanya mema miongoni mwa baba zao na wake zao na watoto wao; bila shaka Wewe ndiye Mwenye nguvu, Mwenye hikima ”

رَبَّنَا وَأَدْخِلْهُمْ جَنَّاتٍ عَدْنٍ الَّتِي وَعَدْتَهُمْ وَمَنْ صَلَحَ مِنْ آبَائِهِمْ وَأَزْوَاجِهِمْ وَذُرِّيَّاتِهِمْ إِنَّكَ أَنْتَ الْعَزِيزُ الْحَكِيمُ ⑩

9. “Na waepushé na maovu, kwani umuepushaye na maovu siku hiyo, hakika umemrehemu; na huko ndiko kufuzu kukubwa.”

وَقِهِمُ السَّيِّئَاتِ وَمَنْ تَقِ السَّيِّئَاتِ يَوْمَئِذٍ فَقَدْ رَحِمْتَهُ وَذَلِكَ هُوَ الْفَوْزُ الْعَظِيمُ ⑪

10. Kwa hakika wale waliokufuru watanadiwa, (wataambiwa): “Bila shaka kukuchukieni Mwenyezi Mungu (wakati mlipokuwa mkimkufuru duniani) ni kukubwa kuliko kujichukia nyinyi (leo) nafsi zenu (humo Motoni). (Kumbukeni) mlipokuwa mnaitwa katika Uislamu na nyinyi mkakufuru!”

إِنَّ الَّذِينَ كَفَرُوا يُبَادُونَ لَمَقْتُ اللَّهِ أَكْبَرُ مِنْ مَقْتِكُمْ أَنْفُسَكُمْ إِذْ تُدْعَوْنَ إِلَى الْإِيمَانِ فَتُكْفَرُونَ ⑫

11. Watasema: “Mola wetu! Umetufisha mara mbili na umetuhuisha mara mbili! Basi tunakiri dhambi zetu. Basi je, iko njia ya kutoka? (Tukarejeza duniani?)” (Wataambiwa: “Hapana!”)

قَالُوا رَبَّنَا آمَنَّا إِثْنَيْنِ وَأَحْيَيْنَا إِثْنَيْنِ فَأَعْتَرَفْنَا بِذُنُوبِنَا فَهَلْ إِلَى خُرُوجٍ مِنْ سَبِيلٍ ⑬

12. “Kwa sababu mlikuwa akitajwa (akiombwa) Mwenyezi Mungu peke yake mnakanusha na akishirikishwa mnaamini. Basi hukumu (leo) ni Yake (Mwenyewe tu) Mwenyezi Mungu aliye juu aliye Mkuu.”

ذِكْرِكُمْ بآيَاتِهِ إِذَا دُعِيَ اللَّهُ وَحْدَهُ كَفَرْتُمْ وَلَنْ يَشْرَكَ بِهِ تَوْمُؤُنُكُمْ فَأَحْكُمِ اللَّهُ الْعَلِيِّ الْكَبِيرِ ⑭

13. Yeye ndiye anayekuonyesheni Ishara zake, (za neema zake) na kukuteremshieni riziki kutoka mbinguni. Na hapana anayekumbuka (kweli kweli) ila anayerejea (kwa Mwenyezi Mungu).

هُوَ الَّذِي يُرِيكُمْ آيَاتِهِ وَيُنزِلُ لَكُمْ مِنَ السَّمَاءِ رِزْقًا وَمَا يَتَذَكَّرُ إِلَّا مَنْ يُنِيبُ ⑮

14. Basi muombeni Mwenyezi Mungu mumfanyie yeye tu ibada yenu, ingawa makafiri watachukiwa.

فَادْعُوا اللَّهَ مُخْلِصِينَ لَهُ الدِّينَ وَلَوْ كَرِهَ الْكَافِرُونَ ⑯

15. Yeye ndiye Mwenye vyeo vya juu kabisa, Mwenye enzi. Hupeleka Wahyi wa amri yake kwa amtakaye miongoni mwa waja Wake ili kuwaonya (viumbe) siku ya kukutana (naye)

رَفِيعِ الدَّرَجَاتِ ذُو الْعَرْشِ يُلْقِي الرُّوحَ مِنْ أَمْرِهِ عَلَى مَنْ يَشَاءُ مِنْ عِبَادِهِ لِيُنذِرَ يَوْمَ التَّلَاقِ ⑰

binaadamu tu. Basi natupunguze deko kwa Mwenyezi Mungu. Kudeka hapa, siko kutakokupatia kucheka huko. Wacha Deko upate Kicheko.

Ya Rabi Twaomba
Kwenye maghorofa
Huyu afurahi
Kwenye hiyo Pepo

Waume wake
Ukatuweke
Yule acheke
Yenye neema.

15. Tazama ubabaishaji wao. Wanajua kuwa *Ar Ruuh* iliyoko hapa ni Wahyi kama walivyosema Wafasiri wote, si Baidhawya tu, kama walivyoonyesha wao. Na ile iliyoko katika ile Aya waliyoifanya ni ya 73 ya *Surat Sad* ni ya Roho kama wanavyosema Wafasiri wote na kama tulivyobainisha huko. Lakini wanababaisha tu.

16. Siku watakayodhihiri (mbele ya Mwenyezi Mungu), na haitafichika habari yao yoyote kwa Mwenyezi Mungu. Leo ufalme ni wa nani? Ni wa Mwenyezi Mungu Mmoja, Mwenye nguvu (za kufanya atakalo).

يَوْمَهُمْ بِرَبْرُودٍ ۗ لَا يُخْفَىٰ عَلَى اللَّهِ مِنْهُمْ شَيْءٌ ۗ
لَمِنَ الْمَلِكِ الْيَوْمَ لِلَّهِ الْوَاحِدِ الْقَهَّارِ ﴿١٦﴾

17. Leo kila mtu atapewa malipo ya yale aliyoyatenda; hakuna dhulma leo, bila shaka Mwenyezi Mungu ni Mwepesi wa kuhisabu.

الْيَوْمَ نُجْزِي كُلَّ نَفْسٍ بِمَا كَسَبَتْ ۗ لَا ظُلْمَ الْيَوْمَ
إِنَّ اللَّهَ سَرِيعُ الْحِسَابِ ﴿١٧﴾

18. Na waonye siku (ya Kiama) ambayo iko karibu mno (na kufika), wakati nyoyo zitakapofika kooni, wamejaa huzuni. Madhalimu hawatakuwa na rafiki, (mpenzi) (siku hiyo) wala muombezi atiiwaye.

وَأَنْذَرَهُمْ يَوْمَ الْأَرْزَاقِ ۖ إِذِ الْقُلُوبُ لَدَى الْحَنَاجِرِ
كَظِيمِينَ ۗ مَا لِلظَّالِمِينَ مِنْ حَمِيمٍ وَلَا شَفِيعٍ
يُطَاعُ ﴿١٨﴾

19. (Mwenyezi Mungu) anajua hiyana ya macho na yanayoficha vifua.

يَعْلَمُ حَافِيَةَ الْأَعْيُنِ وَمَا تُخْفِي الصُّدُورُ ﴿١٩﴾

20. Na Mwenyezi Mungu huhukumu kwa haki; lakini wale wanaowaabudu wasiyokuwa Mwenyezi Mungu hawahukumu chochote; Kwa hakika Mwenyezi Mungu ni Mwenye kusikia, Mwenye kuona.

وَاللَّهُ بِقِصْقِ بِالْحَقِّ وَالَّذِينَ يَدْعُونَ مِنْ دُونِهِ
لَا يَفْضُلُونَ شَيْءًا إِنَّ اللَّهَ هُوَ السَّمِيعُ الْبَصِيرُ ﴿٢٠﴾

21. Je! Hawakusafiri katika nchi wakaona jinsi ulivyokuwa mwisho wa wale waliokuwa kabla yao? Wao walikuwa wenye nguvu zaidi na taathira katika ardhi kuliko hao (Makureshi); na Mwenyezi Mungu aliwatia mkononi kwa sababu ya makosa yao; wala hakukuwa na wa kuwalinda na Mwenyezi Mungu.

أَوَلَمْ يَلْبِسُوا فِي الْأَرْضِ فَيَنْظُرُوا كَيْفَ كَانَ حَاقِبَتَهُ
الَّذِينَ كَانُوا مِنْ قَبْلِهِمْ كَانُوا هُمْ أَشَدَّ مِنْهُمْ قُوَّةً وَ
أَثَارًا فِي الْأَرْضِ فَأَخَذَهُمُ اللَّهُ بِذُنُوبِهِمْ ۗ وَمَا كَانَ
لَهُمْ مِنَ اللَّهِ مِنْ وَاقٍ ﴿٢١﴾

22. Hayo ni kwa sababu walikuwa wanawajia Mitume wao kwa hoja zilizo wazi, lakini wakawakanusha, ndipo Mwenyezi Mungu akawatesa. Bila shaka yeye ni Mwenye nguvu, Mkali wa kuadhibu.

ذَلِكَ بِأَنَّهُمْ كَانَتْ تَأْتِيهِمْ رُسُلُهُمْ بِالْبَيِّنَاتِ فكَفَرُوا
فَأَخَذَهُمُ اللَّهُ بِرَأْسِهِ قَوْمٍ شَدِيدِ الْعِقَابِ ﴿٢٢﴾

23. Na kwa yakini tulimtuma Musa pamoja na miujiza yetu na hoja (dalili) zilizo dhahiri.

وَلَقَدْ أَرْسَلْنَا مُوسَىٰ بِآيَاتِنَا وَسُلْطَانٍ مُبِينٍ ﴿٢٣﴾

24. (Tulimpeleka) kwa Firauni na Hamana na Karuni, wakasema: "(Huyu ni) mchawi, muongo mkubwa."

إِلَىٰ فِرْعَوْنَ وَهَامَانَ وَقَارُونَ فَقَالُوا سِحْرٌ كَذَّابٌ ﴿٢٤﴾

25. Basi alipowaletea haki inayotoka kwetu, walisema: "Waueni watoto wanaume wa wale waliomuamini na wa wacheni hai wanawake wao:" Na vitimbi vya makafiri haviwi ila ni vyenye kuondoka patupu.

فَلَمَّا جَاءَهُمْ بِالْحَقِّ مِنْ عِنْدِنَا قَالُوا اقْتُلُوا
أَبْنَاءَ الَّذِينَ آمَنُوا مَعَهُ وَاسْتَحْيُوا نِسَاءَهُمْ ۗ
وَمَا كَيْدُ الْكٰفِرِينَ إِلَّا فِي ضَلَالٍ ﴿٢٥﴾

23-37. Kisa cha Nabii Musa na Firauni. Wala haipendezi kwa Mwislamu — anapoono vihendo na viroja — akasema: "Ukistaajabu ya Musa utaona ya Firauni. Ukistaajabu ya chawa utaona ya kunguni." Mtume halinganishwi na wabaya. Maneno ya kijinga haya, si ya kiakili wala ya kidini.

26. Na akasema Firauni: "Niachieni nimuue Musa, naye amwite Mola wake! (Amhami). Mimi ninachelea asije kuiharibu dini yenu au kuleta matata katika nchi."

27. Na Musa akasema: "Mimi najikinga kwa Mola wangu na Mola wenu anilinde na kila mwenye jeuri, asiyeamini siku ya Hisabu."

28. Na akasema mtu mmoja Mwislamu aliyekuwa mmoja wa watu wa Firauni afichaye Uislamu wake: "Oh! Mtamuua mtu kwa sababu anasema Mola wangu ni Mwenyezi Mungu? Na kwa yakini yeye amekujieni kwa dalili wazi wazi zitokazo kwa Mola wenu! (Muacheni msimuuwe). Akiwa mwongo, basi uwongo wake ni juu yake mwenyewe, (utamdhuru mwenyewe), na kama akiwa ni mkweli, yatakupatani (papa hapa) baadhi ya hayo anayokuahidini (kuwa yatakupatani papa hapa ulimwenguni). Bila shaka Mwenyezi Mungu hamuongozi yule apindukiaye mipaka, mwongo (mkubwa)."

29. "Enyi watu wangu! Leo mna ufalme, mmeshinda katika ardhi; basi ni nani atakayetusaikia kutuokoa na adhabu ya Mwenyezi Mungu kama ikitufikia?" Firauni akasema: "Sikupeni shauri ila ile niliyoiona (kuwa ni shauri nzuri) wala sikuongozeni ila kwenye njia ya uongofu."

30. Na yule aliyeamini akazidi kusema: "Enyi watu wangu! Hakika mimi nakuhofieni mfano wa siku za (adhabu iliyoyafika hayo) makundi (ya maadui wa Mwenyezi Mungu)"

31. "Mfano wa hali ya watu wa Nuhu na 'Adi na Thamudi na wale waliokuja baada yao. Na Mwenyezi Mungu hataki kuwadhulumu watu (wake)."

32. "Na enyi watu wangu! Kwa yakini nakuhofieni siku ya kuitana, (kupiga makelele kwa adhabu za hiyo siku ya Kiama)"

33. "Siku mtakapogeuka kurudi nyuma (mkimbie, na hamna pa kwenda). Hamtakuwa na mlinzi kwa Mwenyezi Mungu. Na mwenye kuhukumiwa na Mwenyezi Mungu kupotea, basi huyo hana muongozi yoyote.

34. "Na bila shaka zamani alikujieni Yusufu kwa dalili zilizo wazi, lakini nyinyi mliendelea katika

وَقَالَ فِرْعَوْنُ ذُرِّيَّتِي أَقْتُلْ مُوسَى وَلْيَدْعُ رَبَّهُ
إِنِّي أَخَافُ أَنْ يُبَدِّلَ دِينَكُمْ أَوْ أَنْ يُظْهِرَ فِي
الْأَرْضِ الْفَسَادَ ﴿٢٦﴾

وَقَالَ مُوسَى إِنِّي عُذْتُ بِرَبِّي وَرَبِّكُمْ مِنْ كُلِّ مُتَكَبِّرٍ
لَا يُؤْمِنُ بِيَوْمِ الْحِسَابِ ﴿٢٧﴾

وَقَالَ رَجُلٌ مُؤْمِنٌ مِنْ آلِ فِرْعَوْنَ يَكْتُمُ إِيمَانَهُ
أَتَقْتُلُونَ رَجُلًا أَنْ يَقُولَ رَبِّيَ اللَّهُ وَقَدْ جَاءَكُمْ
بِالْبَيِّنَاتِ مِنْ رَبِّكُمْ ۗ وَإِنْ يَكُ كَاذِبًا فَعَلَيْهِ
كَذِبُهُ ۗ وَإِنْ يَكُ صَادِقًا يُصِيبْكُمْ بَعْضُ الَّذِي
يَعِدُّكُمْ إِنَّ اللَّهَ لَا يَهْدِي مَنْ هُوَ مُصِرٌّ كَذَابٌ ﴿٢٨﴾

يَقَوْمَ لَكُمْ الْمَلِكُ الْيَوْمَ ظَهَرِينَ فِي الْأَرْضِ
فَمَنْ يَبْصُرْنَا مِنْ بَآئِسِ اللَّهِ إِنْ جَاءَنَا قَالَ فِرْعَوْنُ
مَا أُرِيكُمْ إِلَّا مَا أَرَىٰ وَمَا أَهْدِيكُمْ إِلَّا سَبِيلَ
الرَّشَادِ ﴿٢٩﴾

وَقَالَ الَّذِي آمَنَ يَقَوْمِ إِنِّي أَخَافُ عَلَيْكُمْ مِثْلَ يَوْمِ
الْأَحْزَابِ ﴿٣٠﴾

مِثْلَ دَابِ قَوْمِ نُوحٍ وَعَادٍ وَثَمُودَ وَالَّذِينَ مِنْ
بَعْدِهِمْ ۗ وَمَا اللَّهُ بِرَبِّدٍ ظَلَمَ الْعِبَادَ ﴿٣١﴾

وَيَقَوْمِ إِنِّي أَخَافُ عَلَيْكُمْ يَوْمَ التَّنَادِ ﴿٣٢﴾

يَوْمَ تَوَلَّوْنَ مُدْبِرِينَ مَا لَكُمْ مِنَ اللَّهِ مِنْ عَاصِمٍ
وَمَنْ يَضِلَّ اللَّهُ فَمَا لَهُ مِنْ هَادٍ ﴿٣٣﴾

وَلَقَدْ جَاءَكُمْ يُوسُفُ مِنْ قَبْلِ الْبَيِّنَاتِ فَمَا زِلْتُمْ

34. Makadiyani katika Aya hii waliyoifanya kuwa ya 35 wametia ule ukafiri wao wa kusema kuwa baada ya Nabii Muhammad ataletwa Mtume mwingine, kama walivyoletwa baada ya Mitume wengine.

snaka kwa yale aliyokuleteeni; mpaka alipofariki mkasema: 'Mwenyezi Mungu hataleta kabisa Mtume baada yake.' Kama hivyo, Mwenyezi Mungu humuacha kupotea yule anayepindukia mipaka katika maasia anayejitia shaka (zisizostahiki).

35. "(Kama hao) ambao wanajadiliana katika Aya za Mwenyezi Mungu pasipo dalili yoyote iliyowajia. Ni chukizo kubwa mbele ya Mwenyezi Mungu na mbele ya wale walioamini (kupinga hizo Aya bure bure). Hivi ndivyo Mwenyezi Mungu apigavyo muhuri juu ya kila moyo wa ajitukuzaye jeuri (akaufanya usisikie lo lote)."

36. Na Firauni akasema: "Ewe Hamana! Nijengee mnara ili nipate kuzifikia njia"

37. "Njia za mbinguni ili nikamuone Mungu wa Musa; na kwa yakini ninamjua kuwa ni muongo tu (huyo Musa, lakini nataka kukuonyesheni na nyinyi)." Na hivi ndivyo Firauni alivyopambiwa ubaya wa vitendo vyake na akazuiliwa njia (ya haki); lakini vitimbi vya Firauni havikuwa ila katika kuangamia tu.

38. Na yule aliyeamini aliendelea kusema: "Enyi watu wangu! Nifuateni, nitakuongozeni njia ya uongofu."

39. "Enyi watu wangu! Kwa hakika maisha ya dunia hii ni starehe (ipitayo tu), na bila shaka Akhera ndiyo nyumba ya kukaa daima."

40. "Afanyaye ubaya hatalipwa ila sawa na huo uwovu wake, na afanyaye wema, akiwa mwanamume au mwanamke, naye ni Mwislamu, basi hao wataingia Peponi, waruzukiwe humo bila hisabu."

41. "Na enyi watu wangu! Kwa nini mimi nakuiteni katika uokofu, nanyi mnaniita kwenye Moto?"

42. "Mnaniita nimkufuru Mwenyezi Mungu na kumshirikisha na yule ambaye simjui, nami nakwiteni kwa Mwenye nguvu (na) Mwingi wa msamaha."

فِي شَاكٍ مِّمَّا جَاءَ كَرِهًا حَتَّىٰ إِذَا هَلَكَ قُلْتُمْ لَنْ يَبْعَثَ اللَّهُ مِنْ بَعْدِهِ رَسُولًا ۚ كَذَٰلِكَ يُضِلُّ اللَّهُ مَنِ هُوَ مُّسْرِفٌ مُّذْتَابٌ ﴿٣٥﴾

الَّذِينَ يُجَادِلُونَ فِي آيَاتِ اللَّهِ يَعْتَدُونَ أَنَّهُمْ كَبُرَ مَقْتًا عِنْدَ اللَّهِ وَعِنْدَ الَّذِينَ آمَنُوا ۚ كَذَٰلِكَ يَضْرِبُ اللَّهُ عَلَىٰ كُلِّ قَلْبٍ مُّتَكَبِّرٍ جُبَابًا ﴿٣٦﴾

وَقَالَ فِرْعَوْنُ يَا هَٰمَانُ ابْنِ لِي صَرْحًا لَّعَلِّي أَبْلُغُ الْأَسْبَابَ ﴿٣٧﴾

أَسْبَابَ السَّمَوَاتِ فَأَطَّلِعَ إِلَىٰ إِلَهِ مُوسَىٰ وَإِنِّي لَأَظُنُّهُ كَاذِبًا ۚ وَكَذَٰلِكَ نُفَصِّلُ لِفِرْعَوْنَ سُوءَ عَمَلِهِ وَصُدَّ عَنِ السَّبِيلِ ۚ وَمَا كَيْدُ فِرْعَوْنَ إِلَّا فِي تَبَابٍ ﴿٣٨﴾

وَقَالَ الَّذِينَ آمَنُوا يَقَوْمِ الْيَهُودِ أَهَدَيْتُمْ سَبِيلَ الرِّشَادِ ﴿٣٩﴾

يَقَوْمِ إِنَّمَا هَٰذِهِ الْحَيَاةُ الدُّنْيَا مَتَاعٌ وَإِنَّ الْآخِرَةَ هِيَ دَارُ الْقَرَارِ ﴿٤٠﴾

مَنْ عَمِلْ سَيِّئَةً فَلَا يُجْزَىٰ إِلَّا مِثْلَهَا وَمَنْ عَمِلْ صَالِحًا مِّنْ دُونِ أَوْ أُنْتَىٰ ۖ وَهُوَ مُؤْمِنٌ فَأُولَٰئِكَ يَدْخُلُونَ الْجَنَّةَ يُرْمَوْنَ فِيهَا بِغَيْرِ حِسَابٍ ﴿٤١﴾ وَيَقَوْمِ مَا لِيَ أَدْعُوكُمْ إِلَى النَّجْوَىٰ وَ تَدْعُونَنِي إِلَى النَّارِ ﴿٤٢﴾

تَدْعُونَنِي لِأَكْفُرَ بِاللَّهِ وَ أُشْرِكَ بِهِ مَا لَيْسَ لِي بِهِ عِلْمٌ ۚ وَإِنَّا أَدْعُوكُمْ إِلَى الْعَزِيزِ الْعَقَّارِ ﴿٤٣﴾

Wanajua — na kila Mwislamu anajua — kuwa Mwenyewe Mwenyezi Mungu ndiye aliyesema kuwa Nabii Muhammad ndiye Mtume wa mwisho, na mwenyewe Mtume akatangaza kuwa hatapewa Utume mtu mwingine baada yake. Na tumeyasema kwa urefu zaidi haya katika Aya ya 40 ya *Suratul Ahzab*.

38. Huyu ni katika jamaa zake Firauni lakini aliyaamini barabara aliyokuja nayo Nabii Musa; akaingia kuwalingania watu kwa hikima na busara na upole. Na hivi ndivyo kulingania kunakohimizwa na Uislamu.

43. "Bila shaka mnaniita kwenda kuwaabudu ambao hawana wito duniani wala katika Akhera, na marejeo yetu ni kwa Mwenyezi Mungu. Na wanaopindukia mipaka (ya Mwenyezi Mungu) hao ndio watu wa Motoni."

44. "Basi karibuni hivi mtayakumbuka ninayokuambieni. Nami ninamkabidhi (namwachia) Mwenyezi Mungu mambo yangu; Hakika Mwenyezi Mungu anawaona waja (wake wote)."

45. Basi Mwenyezi Mungu akamlinda na ubaya wa hila walizozifanya; na adhabu mbaya ikawazunguka hao watu wa Firauni pamoja naye.

46. Adhabu za Motoni wanadhihirishiwa (makaburini mwao) asubuhi na jioni. Na siku ile kitakapotokea Kiama (kutasemwa): "Waingizeni watu wa Firauni katika adhabu kali zaidi (kuliko hii waliyoipata kaburini)."

47. Na (wakumbushe) watakapobishana katika Moto huo — wakati madhaifu watakapowaambia wale waliojitukuza: "Kwa yakini sisi tulikuwa wafuasi wenu, basi je, mnaweza kutuondolea sehemu kidogo ya Moto?"

48. Waseme wale waliokuwa wakijitukuza: "Sisi sote tumo humu; Mwenyezi Mungu amekwishahukumu baina ya viumbe; (na tumekwishastahiki Moto, hatuna la kufanya)."

49. Na wale waliomo Motoni watawaambia walenzi wa Jahanamu: "Muombeni Mola wenu atupunguzie (alau) siku moja ya adhabu."

50. (Walenzi) wawaambie: "Je, hawakuwa wakikujieni Mitume wenu kwa hoja zilizo wazi?" Waseme: "Kwa nini? (Wakitujia lakini tuliasi)" Wawaambie: "Basi ombeni; na madua ya makafiri hayawi ila ni ya kupotea bure."

51. Bila shaka sisi tunawanusuru Mitume wetu na wale walioamini katika maisha ya dunia na siku watakaposimama mashahidi (kushuhudia amali za viumbe)

52. Siku ambayo hautawafaa madhalimu udhuru wao na watapata laana; na mahali pao patakuwa pabaya kabisa.

لَا جَرَمَ أَنَّمَا تَدْعُونَنِي إِلَيْهِ لَيْسَ لَهُ دَعْوَةٌ فِي الدُّنْيَا وَلَا فِي الْآخِرَةِ وَأَنْ مَرَدُّنَا إِلَى اللَّهِ وَأَنَّ الْمُسْرِفِينَ هُمْ أَصْحَابُ النَّارِ ﴿٤٣﴾

فَتَذَكَّرُونَ مَا أَقُولُ لَكُمْ وَأَفِضُ أَمْرِي إِلَى اللَّهِ إِنَّ اللَّهَ بَصِيرٌ بِالْعِبَادِ ﴿٤٤﴾

فَوَقَّعَهُ اللَّهُ سَيِّئَاتٍ مَا مَكَرُوا وَحَاقَ بِآلِ فِرْعَوْنَ سُوءُ الْعَذَابِ ﴿٤٥﴾

النَّارُ يُعْرَضُونَ عَلَيْهَا غُدُوًّا وَعَشِيًّا، وَيَوْمَ تَقُومُ السَّاعَةُ أَدْخِلُوا آلَ فِرْعَوْنَ أَشَدَّ الْعَذَابِ ﴿٤٦﴾

وَإِذْ يَتَخَفَتُونَ فِي النَّارِ فَيَقُولُ الضُّعْفَاءُ لِلَّذِينَ اسْتَكْبَرُوا إِنَّا كُنَّا لَكُمْ تَبَعًا فَهَلْ أَنْتُمْ مُغْنُونَ عَنَّا نَصِيبًا مِنَ النَّارِ ﴿٤٧﴾

قَالَ الَّذِينَ اسْتَكْبَرُوا إِنَّا كُلٌّ فِيهَا إِنَّ اللَّهَ قَدِ احْكَمَ بَيْنَ الْعِبَادِ ﴿٤٨﴾

وَقَالَ الَّذِينَ فِي النَّارِ لِخَدْنَةً جَهَنَّمَ ادْعُوا رَبَّكُمْ يُخَفِّفْ غَنَايَوْمًا مِنَ الْعَذَابِ ﴿٤٩﴾

قَالُوا أَوَلَمْ تَكُ تَأْتِيكُمْ رُسُلُكُمْ بِالْبَيِّنَاتِ، قَالُوا بَلَى، قَالُوا فَادْعُوا، وَمَا دَعْوُ الْكَافِرِينَ إِلَّا فِي ضَلَالٍ ﴿٥٠﴾

إِنَّا لَنَنْصُرُ رُسُلَنَا وَالدِّينَ أَمْوًا فِي الْحَيَاةِ الدُّنْيَا وَيَوْمَ يَقُومُ الْأَشْهَادُ ﴿٥١﴾

يَوْمَ لَا يَنْفَعُ الظَّالِمِينَ مَعَذرتُهُمْ وَلَهُمُ اللَّعْنَةُ وَلَهُمْ سُوءُ الدَّارِ ﴿٥٢﴾

46. Hii ni dalili moja ya kuwa kuna starehe ya Kaburi kwa wema na adhabu kwa wabaya.

51. Wema wasikate tamaa. Watapata nusra tu japo itakawia vipi — na japo baada ya kufa kwao. Ya haki wanayoyalingania yatakuwa tu.

53. Na kwa hakika tulimpa Musa uwongofu na tukawarithisha wana wa Israili Kitabu

54. (Kilichokuwa) Uwongofu na ukumbusho kwa wenye akili.

55. Basi subiri; bila shaka ahadi za Mwenyezi Mungu ni kweli, na omba msamaha kwa dhambi zako, na umtukuze Mola wako na kumsifu jioni na asubuhi.

56. Kwa yakini wale wanaobishana katika Aya za Mwenyezi Mungu pasipo dalili yoyote iliyowajia, hamna nyoyoni mwao ila kiburi, (kutafuta ukubwa); lakini hawataufikia; basi jikinge kwa Mwenyezi Mungu, kwa hakika yeye ni Mwenye kusikia, Mwenye kuona.

57. Kwa yakini umbo la mbingu na ardhi ni kubwa kuliko umbo la wanaadamu. (Basi Mwenyezi Mungu aliyeumbe mbingu na ardhi ndiyo kutamshinda kuwafufua akawapa umbo jingine na uhai mwengine Binaadamu?) Lakini watu wengi hawajui (ila wanajisemea tu).

58. Na kipofu na mwenye macho hawawi sawa, na wale walioamini na kufanya wema (hawawi sawa) na wafanyao uovu. Mnayoyakumbuka ni kidogo kabisa nyinyi.

59. Kwa yakini Kiama kitakuja, nacho hakina shaka; lakini watu wengi hawaamini.

60. Na Mola wenu anasema: "Niombeni nitakujibuni. Kwa hakika wale wajivunao kufanya ibada yangu, bila shaka wataingia Jahanamu, wadhalilike."

61. Mwenyezi Mungu ni yule aliyekufanyieni usiku ili mtulie humo, na mchana wenye nuru (ili muweze kufanya mashughuli yenu). Hakika Mwenyezi Mungu ni mwenye fadhila kubwa kwa watu, lakini watu wengi hawashukuru.

وَلَقَدْ آتَيْنَا مُوسَى الْهُدَىٰ وَأَوْرَثْنَا بَنِي إِسْرَائِيلَ الْكِتَابَ ﴿٥٣﴾

هُدًى لِّمَن ذَكَرَىٰ لِأُولَى الْأَنْبِيَاءِ ﴿٥٤﴾

فَاصْبِرْ إِنَّ وَعْدَ اللَّهِ حَقٌّ ۖ وَاسْتَغْفِرْ لِذَنبِكَ وَسَبِّحْ بِحَمْدِ رَبِّكَ بِالْعَشِيِّ وَالْإِبْكَارِ ﴿٥٥﴾

إِنَّ الَّذِينَ يُجَادِلُونَ فِي آيَاتِ اللَّهِ بِغَيْرِ سُلْطَانٍ أَتَتْهُمْ لَئِن فِي صُدُورِهِمْ إِلَّا كِبْرٌ مَّا هُمْ بِبَالِغِيهِ فَاسْتَعِذْ بِاللَّهِ إِنَّهُ هُوَ السَّمِيعُ الْبَصِيرُ ﴿٥٦﴾

لَخَلْقُ السَّمَوَاتِ وَالْأَرْضِ أَكْبَرُ مِن خَلْقِ النَّاسِ وَلَكِنَّ أَكْثَرَ النَّاسِ لَا يَعْلَمُونَ ﴿٥٧﴾

وَمَا يَسْتَوِي الْأَعْمَىٰ وَالْبَصِيرُ وَالَّذِينَ آمَنُوا وَعَمِلُوا الصَّالِحَاتِ وَلَا الْمَسِيءُ قَلِيلًا ۗ مَّا تَتَذَكَّرُونَ ﴿٥٨﴾

إِنَّ السَّاعَةَ لَأْتِيَةٌ لَا رَيْبَ فِيهَا وَلَكِنَّ أَكْثَرَ النَّاسِ لَا يُؤْمِنُونَ ﴿٥٩﴾

وَقَالَ رَبُّكُمْ ادْعُونِي أَسْتَجِبْ لَكُمْ إِنَّ الَّذِينَ يَسْتَكْبِرُونَ عَنْ عِبَادَتِي سَيَدْخُلُونَ جَهَنَّمَ ذُخْرَيْنَ ﴿٦٠﴾

اللَّهُ الَّذِي جَعَلَ لَكُمْ الْبَيْتَ لِتَسْكُنُوا فِيهِ وَالنَّهَارَ مُبْصِرًا إِنَّ اللَّهَ لَذُو فَضْلٍ عَلَى النَّاسِ وَلَكِنَّ أَكْثَرَ النَّاسِ لَا يَشْكُرُونَ ﴿٦١﴾

60. Anahimiza Mwenyezi Mungu kuombwa yeye — na kuabudiwa yeye vile vile. Basi nazitupwe dua za kuomba makaburi na mizimu na . . .

Nguvu zao na za Mola Bora zipi?

61. Aya hii ni moja katika stishhadi wanazotoa wanaoharimisha KUNADI SALA kabla ya kukurubia wakati wa Alfajiri. Kusinadiwe mbele ya nusu saa kabla ya kuingia wakati wa Alfajiri. Usiku ni wakati wa mapumziko kama alivyokariri Mwenyezi Mungu haya katika Aya nyingi za Sura nyingi, kama Aya hii ya 61 ya Sura hii na Aya ya 86 ya *Suratun Naml* na Aya ya 72 na 73 za *Suratul Qasas* na Aya ya 67 ya *Surat Yunus* na Aya 96 ya *Suratul An-Am* na nyinginezo. Basi wanaonadi Sala mapema — kabla ya nusu saa hivi kabla ya kuingia wakati — wasidhani kuwa wanafanya mema. Wanafanya vibaya. Wataingia katika wale ambao wenyewe wanadhani wanafanya kheri; kumbe wanafanya shari. Na hii ni moja katika khasara zinazowapata wanaotaka kufanya mema bila ya kusoma vilivyo. Kila asiyesoma vilivyo ataharibu tu, na hali ya kuwa mwenyewe anadhani anatengeza.

62. Huyo ndiye Mwenyezi Mungu Mola wenu, Muumba wa kila kitu; hakuna aabudiwaye kwa haki ila yeye; basi mnageuzwa wapi?

ذِكْرُ اللَّهِ رَبِّكُمْ خَالِقِ كُلِّ شَيْءٍ لَّ إِلَٰهَ إِلَّا هُوَ ۚ فَآلَٰهُ تُوْفِكُمْ ۝۳۲

63. Namna hivi ndivyo walivyogeuzwa wale waliokuwa wakizikanusha Aya za Mwenyezi Mungu (mbele huko).

كَذَٰلِكَ يُؤْفِكُ الَّذِينَ كَانُوا يُآيِتُونَ اللَّهَ بِجَهْدٍ وَّوَنٍ ۝۳۳

64. Mwenyezi Mungu ni yule aliyekufanyieni ardhi kuwa mahali penu pa kukaa, na mbingu kuwa dari (isiyoanguka); na akakutieni sura na akazifanya nzuri sura zenu na akakuruzukuni vitu vizuri. Huyo ndiye Mungu, Mola wenu. Basi Mwenye baraka zote hizi ni Mwenyezi Mungu, Mola wa walimwengu wote.

اللَّهُ الَّذِي جَعَلَ لَكُمْ الْأَرْضَ قَرَارًا وَالسَّمَاءَ بِنَاءً ۚ وَصَوَّرَكُمْ فَأَحْسَنَ صُوْرَكُمْ ۚ وَرَزَقَكُمْ مِنَ الطَّيْبَاتِ ۚ ذِكْرُ اللَّهِ رَبِّكُمْ ۚ فَتَبَرَّكَ اللَّهُ رَبُّ الْعَالَمِينَ ۝۳۴

65. Yeye ndiye aliye Hai siku zote; hakuna aabudiwaye kwa haki ila yeye; kwa hivyo muombeni, mumkhalisie (mumtakasie) utii; kwani shukurani zote anastahiki Mwenyezi Mungu, Mola wa viumbe vyote.

هُوَ الَّذِي لَا إِلَٰهَ إِلَّا هُوَ فَادْعُوْهُ مُخْلِصِينَ لَهُ الدِّينَ ۚ الْحَمْدُ لِلَّهِ رَبِّ الْعَالَمِينَ ۝۳۵

66. Sema: "Mimi nimekatazwa kuwaabudu wale mnaowaabudu mkamuacha Mwenyezi Mungu — ziliponijia hoja zilizo dhahiri kutoka kwa Mola wangu. Na nimeamrisha nimnyenyekee Mola wa walimwengu wote."

قُلْ إِنِّي نُهَيْتُ أَنْ أَعْبُدَ الَّذِينَ تَدْعُونَ مِنْ دُونِ اللَّهِ لَمَّا جَاءَنِي الْبَيِّنَاتُ مِنْ رَبِّي وَأُمِرْتُ أَنْ أُسَلِّمَ لِلرَّبِّ الْعَالَمِينَ ۝۳۶

67. Yeye ndiye aliyekuumbeni kwa udongo, kisha kwa tone la manii, kisha kwa pande la damu, halafu akakutoeni katika hali ya mtoto mchanga; kisha (akakuwacheni) ili mpate kufikilia wakati wa nguvu zenu kamili; kisha muwe wazee. Na wengine katika nyinyi hufishwa kabla (ya kufikia uzee). Na ili mfikie muda uliowekwa (wa kuondoka ulimwengu mumefanyiwa haya) ili mupate kufahamu.

هُوَ الَّذِي خَلَقَكُمْ مِنْ تَرَابٍ ثُمَّ مِنْ نُطْفَةٍ ثُمَّ مِنْ عَلَقَةٍ ثُمَّ يُخْرِجُكُمْ طِفْلًا ثُمَّ لِتَبْلُغُوا أَشُدَّكُمْ ثُمَّ لِتَكُونُوا شُيُوْحًا ۚ وَمِنْكُمْ مَنْ يُتَوَقَّىٰ مِنْ قَبْلُ وَلِتَبْلُغُوا أَجَلًا مُّسَدَّدًا ۚ فَاعْلَمُوا ۝۳۷

68. Yeye ndiye anayehuisa na kufisha, na anapolihukumia jambo (liwe), basi (mara moja tu) huliambia "Kuwa," nalo likawa.

هُوَ الَّذِي يُحْيِي وَيُمِيتُ ۚ فَإِذَا قَضَىٰ أَمْرًا فَإِنَّمَا يَقُولُ لَهُ كُنْ فَيَكُونُ ۝۳۸

69. Je! Huwaoni wale wanaobishana katika Aya za Mwenyezi Mungu? Wanageuziwa wapi, (na haki ndiyo hii)?

الَّذِينَ تَرَاءَى الَّذِينَ يَجَادِلُونَ فِي آيَاتِ اللَّهِ ثُمَّ لَا يُبْصِرُونَ ۝۳۹

70. Ambao wamekadhibisha Kitabu na yale tuliyowatuma nayo Mitume wetu, lakini Karibuni hivi watajua

الَّذِينَ كَذَّبُوا بِالْكِتَابِ وَمَا أَرْسَلْنَا بِهِ رُسُلَنَا فَتَوْفَ يَعْلَمُونَ ۝۴۰

71. Zitakapokuwa pingu shingoni mwao na minyororo (miguuni mwao), wanabururwa

إِذِ الْأَعْلَىٰ فِي أَعْنَاقِهِمْ وَالسَّلْسَلُ يُسْحَبُونَ ۝۴۱

72. Katika maji ya moto, kisha wanaunguzwa Motoni.

فِي الْحَمِيمِ ۚ ثُمَّ فِي النَّارِ يُسْجَرُونَ ۝۴۲

73. Tena wataambiwa: "Wako wapi mliokuwa mkiwashirikisha "

74. "Badala ya Mwenyezi Mungu?" Waseme: "Warnetupotea, bali toka zamani hatukuwa tunamuabudu (yoyote ila wewe)." Namna hivi Mwenyezi Mungu anawaachia makafiri wapotee mbali, (kwa kuwa wanafanya ukaidi).

75. "Haya (yaliyokupatani leo Motoni) ni kwa sababu mlikuwa mkitakabari katika ardhi pasipo haki, na kwa sababu mlikuwa mkijivuna."

76. "Ingieni katika milango ya Jahanamu mkakae humo milele; basi ni mabaya yalioje makazi ya wanaotakabari!"

77. Basi subiri, hakika ahadi ya Mwenyezi Mungu ni kweli. Na kama tukikuonyesha baadhi ya yale tuliyowaahidi au tukikufisha (kabla hujayaona, hapana shaka kuwa yatakuja, kwani wote) watarudishwa kwetu.

78. Na kwa yakini tuliwatuma Mitume kabla yako. Wengine katika hao tumekusimulia (majina yao na habari zao), na wengine hatukukusimulia; na haikuwa kwa Mtume yoyote kuleta Muujiza wowote ila kwa idhini ya Mwenyezi Mungu. Na itakapokuja hukumu ya Mwenyezi Mungu kutahukumiwa kwa haki; na wafanyao mambo ya batili watapata hasara wakati huo.

79. Mwenyezi Mungu ni yule aliyekufanyieni wanyama ili muwapande baadhi yao; na wengine wao muwale.

80. Na katika hao mnayo manufaa (mengi mengi), na mnapata kwao haja zilizomo vifuani mwenu; na mnachukuliwa juu yao, na juu ya marikebu.

81. Naye anakuonyesheni (daima) alama (za neema) zake: basi mnakanusha ipi katika neema za Mwenyezi Mungu (kuwa si neema yake au si neema kamwe)?

82. Je! Hawakusafiri katika ardhi wakaona ulikuwaje mwisho wa wale waliokuwa kabla yao? Wao walikuwa wengi kuliko hawa (Makureshi) na zaidi katika nguvu na katika majengo ardhini; wala hayakuwafaa hayo waliyokuwa wakiyafanya.

83. Basi walipowajia Mitume wao kwa dalili zilizo wazi walifurahia ilimu waliyokuwa nayo (yakujua mambo ya kidunia, wakayapuuza hayo

ثُمَّ قِيلَ لَهُمْ أَيْنَ مَا كُنْتُمْ تُشْرِكُونَ ﴿٧٣﴾

مِنْ دُونِ اللَّهِ قَالُوا ضَلُّوا عَنَّا بَلْ لَمْ نَكُنْ نَدْعُوا مِنْ قَبْلُ شَيْئًا كَذَلِكَ يَضِلُّ اللَّهُ الْكَافِرِينَ ﴿٧٤﴾

ذَلِكُمْ بِمَا كُنْتُمْ تَفْرَحُونَ فِي الْأَرْضِ بِغَيْرِ الْحَقِّ وَبِمَا كُنْتُمْ تَمْرَحُونَ ﴿٧٥﴾

أَدْخُلُوا أَبْوَابَ جَهَنَّمَ خَالِدِينَ فِيهَا فَبِئْسَ مَثْوَى الْمُتَكَبِّرِينَ ﴿٧٦﴾

فَأَصْبِرْ إِنَّ وَعْدَ اللَّهِ حَقٌّ فَإِمَّا نُرَبِّيكَ بِعَظْصِ الْأَرْضِ نَعِدُكَ أَوْ نَوَفِّيكَ فَإِنَّا يَرْجِعُونَ ﴿٧٧﴾

وَلَقَدْ أَرْسَلْنَا رُسُلًا مِنْ قَبْلِكَ مِنْهُمْ مَنْ قَصَصْنَا عَلَيْكَ وَمِنْهُمْ مَنْ لَمْ نَقْصُصْ عَلَيْكَ وَمَا كَانَ لِرَسُولٍ أَنْ يَأْتِيَ بِآيَةٍ إِلَّا بِإِذْنِ اللَّهِ فَإِذَا جَاءَ أَمْرُ اللَّهِ فَخِصْ بِالْحَقِّ وَخَسِرْ هُنَالِكَ الْمُبْطِلُونَ ﴿٧٨﴾

اللَّهُ الَّذِي جَعَلَ لَكُمْ الْأَنْعَامَ لِتَرْكَبُوا مِنْهَا وَمِنْهَا تَأْكُلُونَ ﴿٧٩﴾

وَلَكُمْ فِيهَا مَنَافِعُ وَلِتَبْلُغُوا عَلَيْهَا حَاجَةً فِي صُدُورِكُمْ وَعَلَيْهَا وَعَلَى الْفَالِكِ تَحْمِلُونَ ﴿٨٠﴾

وَيُرِيكُمْ آيَاتِهِ فَأَلَيْتُمْ آيَاتِ اللَّهِ تَتَكَبَّرُونَ ﴿٨١﴾

أَفَلَمْ يَسِيرُوا فِي الْأَرْضِ فَيَنْظُرُوا كَيْفَ كَانَ عَاقِبَةُ الَّذِينَ مِنْ قَبْلِهِمْ كَانُوا أَكْثَرَ مِنْهُمْ وَأَشَدَّ قُوَّةً وَأَثَارًا فِي الْأَرْضِ فَمَا أَعْنَى عَنْهُمْ مَا كَانُوا يَكْسِبُونَ ﴿٨٢﴾

فَلَمَّا جَاءَتْهُمْ رُسُلُهُمْ بِالْبَيِّنَاتِ فَرِحُوا بِمَا عِنْدَهُمْ مِنَ الْعِلْمِ

waliyokuja nayo Mitume). Basi yakawazunguka waliyokuwa wakiyafanyia maskhara.


84. Walipoiona adhabu yetu walisema: "Tunamuamini (sasa) Mwenyezi Mungu kuwa ni wa peke yake na tunaikanusha (miungu) tuliokuwa tukiishirikisha naye."

85. Lakini imani yao haikuwa yenye kuwafaa huu wakati ambao wamekwisha kuiona adhabu yetu. (Hii ni kawaida ya Mwenyezi Mungu iliyopita katika waja wake (wote, kuwa ikishakuja adhabu haikubaliwi toba tena). Na hapo waliokufuru wakapata hasara.

وَ حَاقَ بِهِمْ مَا كَانُوا بِهِ يَسْتَهْزِءُونَ ﴿١٧﴾

فَلَمَّا رَأَوْا بَأْسَنَا قَالُوا آمَنَّا بِاللَّهِ وَحَدَّهُ وَكَفَرْنَا
بِمَا كُنَّا بِهِ مُشْرِكِينَ ﴿١٨﴾

فَلَمَّ يَكُ يَنْفَعُهُمْ إِيمَانُهُمْ لَنَا رَأَوْا بَأْسَنَا
سُنَّتَ اللَّهِ الَّتِي قَدْ خَلَتْ فِي عِبَادِهِ
وَ خَسِرَ هُنَالِكَ الْكَافِرُونَ ﴿١٩﴾



Ina Aya 54

SURAT HAA MYM SAJDAH

Ina Makara 6

(Imeteremka Makka)

Kwa jina la Mwenyezi Mungu, Mwenye kuneemesha neema kubwa kubwa na Mwenye kuneemesha neema ndogo ndogo.

1. Haa Mym.
2. Uteremsho (huu) umetoka kwa (Mwenyezi Mungu) Mwingi wa rehema, Mwingi wa ukarimu.
3. (Hiki ni) Kitabu kinachopambanuliwa (vizuri kabisa) Aya zake. Ni kisomi (kilichoteremka) kwa (lugha ya) Kiarabu kwa watu wanaojua (kheri yao)
4. Kitoacho habari njema na kionyacho, lakini wengi katika wao (Makureshi) wamekengeuka; kwa hivyo hawasikii.
5. Na wakasema: "Nyoyo zetu zi katika vifuniko kwa yale unayotuitia; na katika masikio yetu muna uzito; na baina yetu na baina yako kuna pazia; basi fanya (yako), na sisi tunafanya (yetu; kila mtu asimuingilie mwenziwe)."
6. Sema: "Bila shaka mimi ni mtu kama nyinyi; ninaletewa wahyi (inafunuliwa kwangu) ya kwamba Mungu wenu ni Mungu Mmoja tu. Basi tengeneeni (kwa kufuata haya yanayotoka) Kwake, na mumtake samahani, na adhabu itawapata wanaomshirikisha (Mwenyezi Mungu)"
7. Ambao hawatoi Zaka na wanaikanusha Akhera.

8. Wale wanaoamini na kutenda mema utakuwa kwao ujira usiokoma.

9. Sema: "Oh! Mnamkanusha yule (Mwenyezi Mungu) aliyumba ardhi katika siku mbili (tu), na mnampa washirika? Huyu ndiye Mola wa walimwengu wote. (Mshirika huyo ametoka wapi)."

10. Na akaweka humo milima juu yake (ya uso wake), na akabarikia humo na akakadiria humo

بِسْمِ اللَّهِ الرَّحْمَنِ الرَّحِيمِ

حَمْدٌ

تَنْزِيلٌ مِنَ الرَّحْمَنِ الرَّحِيمِ

كِتَابٌ فَصَّلْتَ آيَاتَهُ قُرْآنًا عَرَبِيًّا لِقَوْمٍ

يَعْلَمُونَ

بَشِيرًا وَنَذِيرًا، فَأَعْرَضَ أَكْثَرُهُمْ فَهُمْ لَا يَسْمَعُونَ

وَقَالُوا قُلُوبُنَا فِي أَكْثَرِ مَا تَدْعُونَا إِلَيْهِ وَ

فِي آذَانِنَا وَقَدْ وُضِعَ بَيْنَنَا وَبَيْنِكَ حِجَابٌ

فَاعْمَلْ إِنَّا عُمَّلُونَ

قُلْ إِنَّمَا أَنَا بَشَرٌ مِثْلُكُمْ يُوحَى إِلَيَّ أَنَّمَا إِلَهُكُمُ

إِلَهُ وَاحِدٌ فَاسْتَقِيمُوا إِلَيْهِ وَاسْتَغْفِرُوا

وَوَيْلٌ لِلشَّارِكِينَ

الَّذِينَ لَا يُؤْتُونَ الزَّكَاةَ وَهُمْ بِالْآخِرَةِ هُمْ

كَافِرُونَ

إِنَّ الَّذِينَ آمَنُوا وَعَمِلُوا الصَّالِحَاتِ لَهُمْ أَجْرٌ

عَظِيمٌ

قُلْ أَيُّكُمْ لَنْتَكْفُرُونَ بِالَّذِي خَلَقَ الْأَرْضَ

فِي يَوْمَيْنِ وَتَجْعَلُونَ لَهُ آندَادًا ذَلِكَ

رَبُّ الْعَالَمِينَ

وَجَعَلَ فِيهَا رَوَاسِيًا مِنْ فَوْقِهَا وَبَرَكَ فِيهَا

5. Visingizio vyao vya uwongo vya kuyakataa yaliyoletwa na Uislamu. Hawana vifuniko, hawana chochote. 9, 10. Tumebainisha katika Aya ya 4 ya *Suratus Sajda* muradi wa hizi siku anazozitaja Mwenyezi Mungu katika muda wa kuumba mbingu na ardhi.

chakula chake (cha kuwatosha watakaokaa humo. Ameyafanya haya) katika siku nne, (mida mine). Haya ni sawa kabisa kwa hao wanaouliza (mambo wakataka kuyajua).

11. Kisha akazielekea mbingu na zilikuwa moshi, basi, akaziambia (mbingu) na ardhi: "Njooni, mkipenda msipende." Vyote viwili vikasema: "Tumekuja, hali ya kuwa wenye utifu."

12. Basi akazifanya mbingu saba katika siku mbili, na kila uwingu akaufunulia kazi yake. Na tumeupamba uwingu wa karibu yenu huu kwa mataa na kuulinda. Hiki ndicho kipimo cha Mwenye nguvu, Mwenye kujua.

13. Basi kama wakipuza sema "Nakuhadharisheni adhabu mfano wa adhabu, (inayoshihi adhabu) ya Adi na Thamudi."

14. Walipowajia Mitume mbele yao na nyuma yao, (wakawaambia): "Msimuabudu ila Mwenyezi Mungu." Wakasema: "Angalitaka Mola wetu (kuleta mjumbe wake) bila shaka angeteremsha Malaika (sio nyinyi wanaadamu wenzetu) Na hakika sisi tunayakanusha mliyotumwa nayo."

15. Basi Adi walitakabari katika ardhi bila ya haki na wakasema. "Ni nani aliye na nguvu zaidi kuliko sisi?" Je! hawakuona ya kwamba Mwenyezi Mungu aliyewaumba wao ni Mwenye nguvu zaidi kuliko wao? Wakawa wanazikanusha Aya zetu.

16. Basi tuliwapelekea kimbunga (upepo mkali) katika siku za shari (yao) ili tuwaonjeshe adhabu ya hizaya (fedheha) katika maisha ya dunia; na bila shaka adhabu ya Akhera ni ya kufedhehesha zaidi; nao hawatanusuriwa (siku hiyo).

17. Na Thamudi tuliwaongoza lakini walipenda upofu kuliko uongofu. Basi uliwatoa roho moto wa adhabu idhalilishayo, kwa sababu ya yale waliyokuwa wakiyachuma.

18. Na tukawaokoa wale walioamini na waliokuwa wakijilinda (na mabaya).

13. Mtume s.a.w. alimsomea mkubwa wa Maqureshi — Utba bin Rabia — mwanzo wa Sura hii. Hata alipofika hapa, Utba akamziba kinywa Mtume kwa khofu iliyompanda. Akenda zake mbio, na Uislamu umekwishanza kumingia moyoni mwake; akawazungumzia wakubwa wenzake. Lakini Abu Jahili na wenziwe walimpandisha mori wa kijahili mpaka akaitoa azma ile. Akafa ukafirini katika vita vya Badri kama alivyokufa Abu Jahli na wafujaji wenzake.

17. Hapa Mwenyezi Mungu anabainisha kuwa amewaongoa, lakini wenyewe wamekataa kufuata.

وَقَدَّرَ فِيهَا أَمْوَانَهَا فِي أَرْبَعَةِ أَيَّامٍ
سَوَاءً لِّلنَّاسِ يَلِيجُ ۝١٠

ثُمَّ اسْتَوَىٰ إِلَى السَّمَاءِ وَهِيَ دُخَانٌ فَقَالَ
لَهَا وَإِلَى الْأَرْضِ إِنِّي نَطُومٌ أَدْرِكِهَا ۚ قَالَ
أَنبَيْنَا طَائِعِينَ ۝١١

فَقَضَيْنَ سَبْعَ سَمَوَاتٍ فِي يَوْمَيْنِ وَأَوْحَىٰ
فِي كُلِّ سَمَاءٍ أَمْرَهَا ۚ وَزَيَّنَّا السَّمَاءَ الدُّنْيَا
بِبَصَائِجٍ ۚ وَحِفْظٍ ۚ ذَٰلِكَ تَقْدِيرُ الْعَزِيزِ
الْعَلِيمِ ۝١٢

فَإِنِ اعْرَضُوا فَعُلْنَا لَهُمُ صُغُورًا ۚ وَثَلَاثَ
صُغُورًا عَادُوا ۚ ثُمَّ دُفِّنُوا ۝١٣

إِذْ جَاءَ نَوْمُ الرُّسُلِ مِنْ بَيْنِ أَيْدِيهِمْ
وَمِنْ خَلْفِهِمْ أَلَّا تَعْبُدُوا إِلَّا اللَّهَ ۚ قَالُوا لَوْ شَاءَ
رَبُّنَا لَأَنزَلَ مَلَائِكَةً فَأِنَّا بِمَا أُرْسِلْتُمْ بِهِ
كٰفِرُونَ ۝١٤

فَأَمَّا عَادُ فَاسْتَكْبَرُوا فِي الْأَرْضِ بِغَيْرِ الْحَقِّ
وَقَالُوا مَنْ أَشَدُّ مِنَّا قُوَّةً ۚ أَوَلَمْ يَرَوْا أَنَّ
اللَّهَ الَّذِي خَلَقَهُمْ هُوَ أَشَدُّ مِنْهُمْ قُوَّةً ۚ وَكَانُوا
بِآيَاتِنَا يَجْحَدُونَ ۝١٥

فَأَرْسَلْنَا عَلَيْهِمْ رِيحًا صَرْصَرًا فِي أَيَّامٍ نَّحْسَاتٍ
لِّنُذِقَهُمُ عَذَابَ الْخَيْرِ فِي الْحَيَاةِ الدُّنْيَا
وَلَعَذَابُ الْآخِرَةِ أَحْزَنُ ۚ وَهُمْ لَا يُبْصِرُونَ ۝١٦
وَأَمَّا ثَمُودُ فَهَدَيْنَاهُمْ فَاسْتَحَبُّوا الْعَنَىٰ عَلَى الْهُدَىٰ
فَأَخَذَتْهُمُ صُغُورَةُ الْعَذَابِ الْهُونِ بِمَا كَانُوا
يَكْسِبُونَ ۝١٧

وَنَجَّيْنَا الَّذِينَ آمَنُوا وَكَانُوا يَتَّقُونَ ۝١٨

19. Na (wakumbushe) siku watakapokusanywa maadui wa Mwenyezi Mungu katika Moto, wakawa wanatengwa makundi mbali mbali.

20. Hata watakapoujia (huo Moto), hapo ndipo masikio yao, na macho yao na ngozi zao (viungo vyao vyengine) zitakapotoa ushahidi juu yao kwa yale waliyokuwa wakiyatenda.

21. Na wao waziambie (hizi) ngozi zao: "Mbona mnatushuhudia?" Nazo ziwaambie: "Mwenyezi Mungu aliyekitamkisha kila kitu ndiye aliyetutamkisha, naye ndiye aliyekuumbeni mara ya kwanza. Na kwake (hivi sasa) mnarudishwa.

22. "Na hamkuwa mukijificha hata masikio yenu na macho yenu na ngozi zenu (viungo vyao vyengine) zisiweze kutoa ushahidi juu yenu; bali mlidhani ya kwamba Mwenyezi Mungu hayajui mengi katika (hayo) mnayoyafanya.

23. "Basi hiyo dhana yenu mliyokuwa mkimdhania Mola wenu imekuangamizeni; na mume kuwa miongoni mwa wenye kukhasirika."

24. Basi wakistahamili, Moto ndiyo maskani yao (na wakitostahamili pia Moto ndio maskani yao); na kama wakitoa udhuru hawatakuwa miongoni mwa wanaokubaliwa nyudhuru zao.

25. Na tukawawekea marafiki waliowapambia yale yaliyo mbele yao na nyuma yao (kuwa 'Msiogope lolote, hakuna chochote huko Akhera'). Basi ikawathubutikia kauli (ya kuadhibiwa Motoni), wawe pamoja na yale mataifa yaliyopita kabla yao, miongoni mwa majini na watu. Hakika wamekuwa ni wenye kuhasirika.

26. Na walisema waliokufuru (kuambizana wenyewe kwa wenyewe):— "Msisikilize Qurani hii (inaposomwa, isije ikakupotezeni) na ipigieni makelele (isomwapo); huenda mkashinda (akawachilia mbali huu uzushi wake)."

27. Basi hao waliokufuru tutawaonjesha adhabu kali na tutawalipa malipo mabaya ya yale waliyokuwa wakiyafanya.

28. Hayo ndiyo malipo ya maadui wa Mwenyezi Mungu — Moto; humo watakuwa na maskani ya maisha; ndiyo malipo (yao) kwa sababu walikuwa wakikufuru Aya zetu.

وَيَوْمَ يُعْشَرُ أَعْدَاءُ اللَّهِ إِلَى النَّارِ فَهُمْ يُوزَعُونَ ﴿١٩﴾

حَتَّىٰ إِذَا مَا جَاءُوهَا شَهِدَ عَلَيْهِمْ سَمْعُهُمْ وَأَبْصَارُهُمْ وَجُلُودُهُم بِمَا كَانُوا يَعْمَلُونَ ﴿٢٠﴾

وَقَالُوا لَوْلَا جُودُهُمْ لِمَ شَهِدْتُمْ عَلَيْنَا قَالَ لَوْ أَنَّا نَطَقْنَا اللَّهُ الَّذِي أَنْطَقَ كُلَّ شَيْءٍ وَهُوَ خَلَقَكُمْ أَوَّلَ مَرَّةٍ وَإِلَيْهِ تُرْجَعُونَ ﴿٢١﴾

وَمَا كُنْتُمْ تَسْتَشِيرُونَ أَن يَشْهَدَ عَلَيْكُمْ سَمْعُكُمْ وَلَا أَبْصَارُكُمْ وَلَا جُلُودُكُمْ وَلَكِنْ ظَنَنْتُمْ أَنَّ اللَّهَ لَا يَعْلَمُ كَثِيرًا مِّمَّا تَعْمَلُونَ ﴿٢٢﴾

وَذَلِكُمْ ظَنُّكُمُ الَّذِي ظَنَنْتُمْ بِرَبِّكُمْ أَرَأَيْتُمْ فَاصِّبْتُمْ مِنْ حُسْرَيْنِ ﴿٢٣﴾

فَإِنْ يَصْبِرُوا فَالنَّارُ مَثْوًى لَهُمْ وَإِنْ يَسْتَعْتِبُوا فَمَا هُمْ مِنَ الْمُعْتَبِينَ ﴿٢٤﴾

وَقَبَضْنَا لَهُمْ فُرُجَاءَ فَرَأَوْهُم مَّا بَيْنَ أَيْدِيهِمْ وَمَا خَلْفَهُمْ وَ حَقَّ عَلَيْهِمُ الْقَوْلُ فِي أُمِّ قَدْحَ حَلَكْتَ مِنْ قَبْلِهِمْ مِنَ الْجِنَّ وَالْإِنْسِ إِنَّهُمْ كَانُوا حُسْرَيْنِ ﴿٢٥﴾

وَقَالَ الَّذِينَ كَفَرُوا لَا تَسْمَعُوا لِهَذَا الْقُرْآنِ وَالْقَوَاعِيهِ كَلَّاكُمْ تَعْلَبُونَ ﴿٢٦﴾

فَلَنْذِيقَنَّ الَّذِينَ كَفَرُوا عَذَابًا شَدِيدًا وَلَنْجَزِيَنَّهُمْ أَثْوَا الَّذِي كَانُوا يَعْمَلُونَ ﴿٢٧﴾

ذَلِكَ جَزَاءُ أَعْدَاءِ اللَّهِ النَّارِ لَهُمْ فِيهَا دَارُ الْخُلْدِ جَزَاءً بِمَا كَانُوا بِآيَاتِنَا يَجْحَدُونَ ﴿٢٨﴾

29. Na wale waliokufuru watasema (katika kutiliana chonza): "Mola wetu! Tuonyeshe wale waliotupoteza miongoni mwa majini na watu ili tuwaweke chini ya miguu yetu, wapate kuwa miongoni mwa walio chini kabisa."

30. Wale waliosema: "Mola wetu ni Mwenyezi Mungu," kisha wakenda mwendo mzuri, hao huwateremkia Malaika (wakati wakitoka roho wakawaambia): "MsioCOPE wala msihuzunike, na furahini kwa Pepo mliyokuwa mkiahidiwa."

31. "Sisi ni vipenzi vyenu katika maisha ya dunia na (huku) katika Akhera, na humo mtapata vitu vinavyopendwa na nafsi zenu, na humo, mtapata mtakavyovitaka."

32. Ni karamu itokayo kwa (Mwenyezi Mungu) Mwingi wa kusamehe (na) Mwingi wa kurehemu.

33. Na ni nani asemaye kauli bora zaidi kuliko aitaye (viumbe) kwa Mwenyezi Mungu, na (mwenyewe) akafanya vitendo vizuri na husema (kwa maneno yake na vitendo vyake): "Hakika mimi ni miongoni mwa Waislamu, (kwa hivyo niko pamoja nao kwa kila jambo)."

34. Mambo mazuri na mabaya hayawi sawa. Ondosha (ubaya unaofanyiwa kwa mema); tahamaki yule ambaye baina yako na baina yake kuna uadui atakuwa kama ni jamaa (yako) mwenye kukufia uchungu.

35. Lakini (jambo hili) hawatapewa ila wale wanaosubiri, wala hawatapewa ila wenye hadhi kubwa (kwa Mwenyezi Mungu).

36. Na kama shetani akikushawishi kwa tashwishi (zake ili ugombane na hao wanaokufanyia ubaya), wewe jikinge kwa Mwenyezi Mungu (kwa kusema): "Audhu Billahi Minash Shaytani Rajym" yeye ni mwenye kusikia, mwenye kujua.

37. Na katika alama zake (za Uungu wake Mwenyezi Mungu) ni (huku kupatikana) usiku na mchana na jua na mwezi; basi msilisujudie jua wala mwezi; bali msujudieni Mwenyezi Mungu aliyeviumba; ikiwa nyinyi mnamuabudu Yeye (basi fanyeni hivi).

وَقَالَ الَّذِينَ كَفَرُوا رَبَّنَا أَرِنَا الَّذِينَ اصَّلْنَا
مِنَ الْجِنِّ وَالْإِنسِ نَجْمَهُمَا تَحْتًا أَفَدَامَنَا
يَكُونُوا مِنَ الْاسْقَلِينَ ﴿٢٩﴾

إِنَّ الَّذِينَ قَالُوا رَبُّنَا اللَّهُ ثُمَّ اسْتَفْتَمُوا
تَتَنَزَّلُ عَلَيْهِمُ الْمَلَائِكَةُ أَلَّا تَخَافُوا وَلَا
تَحْزَنُوا وَابْتَهِرُوا بِالْبَيْتِ الَّذِي كُنْتُمْ تُوعَدُونَ ﴿٣٠﴾

وَكُنْ أَوْلَىٰكُمْ فِي الْحَيَاةِ الدُّنْيَا وَفِي الْآخِرَةِ
وَلَكُمْ فِيهَا مَا نَشْتَهُ أَنفُسُكُمْ وَلَكُمْ فِيهَا
مَا تَدَّعَوْنَ ﴿٣١﴾

يُعْزِزُكُمْ مِّنْ عَفْوِ رَبِّهِمْ ﴿٣٢﴾

وَمَنْ أَحْسَنُ قَوْلًا مِّمَّنْ دَعَا إِلَى اللَّهِ وَعَمِلَ
صَالِحًا وَقَالَ إِنِّي مِنَ الْمُسْلِمِينَ ﴿٣٣﴾

وَلَا تَنْتَوِي الْحَسَنَةَ وَلَا السَّيِّئَةَ، إِرَادَ قَوْلِهَا بِأَلَّتِي هِيَ
أَحْسَنُ فَإِذَا الَّذِي بَيْنَكَ وَبَيْنَهُ عَدَاوَةٌ
كَانَ فِي حَمِيمٍ ﴿٣٤﴾

وَمَا يُلْقِيهَا إِلَّا الَّذِينَ صَبَرُوا، وَمَا يُلْقِيهَا إِلَّا
ذُو حِظٍّ عَظِيمٍ ﴿٣٥﴾

وَأَمَّا يَتَرَعَّتْكَ مِنَ الشَّيْطَانِ نَزْوٌ فَاسْتَعِذْ بِاللَّهِ
إِنَّهُ هُوَ السَّمِيعُ الْعَلِيمُ ﴿٣٦﴾

وَمِنَ آيَاتِهِ الْبَلُّ وَالنَّهَارُ وَاللَّيْلُ وَالْقَمَرُ
لَا تَسْجُدُوا لِلشَّمْسِ وَلَا لِلْقَمَرِ وَاسْجُدُوا لِلَّهِ الَّذِي
خَلَقَهُنَّ إِن كُنْتُمْ إِيَّاهُ تَعْبُدُونَ ﴿٣٧﴾

22. Mulifanya hayo mabaya ndipo vikakushuhudilieni, na lau mungejipusha na hayo visingelikushuhudilieni.

33. Hapana bora kuliko hili: (a) La kuwalingania watu katika Uislamu; na (b) Akawa mwenyewe anafanya mema; na (c) Akawa pamoja kweli kweli na Waislamu wenziwe kwa yao yote.

34-36. Haya tumeyasema mara nyingi sana.

38. Na kama wakitakabari, (basi Mwenyezi Mungu hana haja nao) kwani hao (viumbe watukufu) — (Malaika) — walioko kwake Mola wako wanamsabihi usiku na mchana, wala hawachoki. (Basi kama nyinyi hamuabudu yadhuru nini?)

39. Na katika Ishara zake (kuwa yuko Mwenyezi Mungu) ni kwamba unaiona ardhi imedhalilika (kwa kukosa mvua), lakini tunapoiteremshia maji mara unaiona inataharaki na kuumuka; bila shaka aliyehuisa Ndiye atakayehuisa waliokufa. Hakika Yeye ndiye Mwenye Uweza juu ya kila kitu.

40. Kwa yakini wale wanaozisopotoa Aya zetu (ili wasizifuate na wapoteze watu) hawatufichikii, (tunawajua). Je! Atakayetupwa Motoni ni bora au atakayekuja kwa amani siku ya Kiama? Fanyeni mnavyopenda, kwa yakini Yeye anayaona yote mnavoyafanya.

41. Kwa hakika wale wanaoyakanusha mawaidha yanapowajia (tutawaadhibu). Bila shaka hicho ni Kitabu kihishimiwacho.

42. Haitakifikia batili mbele yake waia nyuma yake; kimeteremshwa na Mwenye hikima, ahimidiwaye.

43. Huambiwi (na hawa makafiri) ila yale yale waliyoambiwa Mitume wa kabla yako; kwa yakini Mola wako ni Mwenye msamaha na Mwenye adhabu iumizayo.

44. Na lau kama tungaliifanya Qurani kwa lugha isiyo ya Kiarabu wangalisema: “Kwa nini Aya zake hazikupambanuliwa? Lo! Lugha isiyokuwa ya Kiarabu na (Mtume) Muarabu! (Mambo gani haya)!” Sema: “Hii (Qurani) ni uwongofu na poza kwa wale walioamini; na wale wasioamini umo uzito katika masikio yao; na hiyo (Qurani) ni giza kwao. (Hawasikii. Kama kwamba) hao wanaitwa, na hali ya kuwa wako mbali kabisa.”

45. Na hakika tulimpa Musa Kitabu lakini kukahitalifiwa kwacho; na lau isingekuwa kauli iliyotangulia kutoka kwa Mola wako (kuwa hukumu ni Akhera), basi wangehukumikiwa (sasa hivi). Na wao wamo katika shaka yenye kuwatia wasiwasi wa haya (aliyokuja nayo Nabii Muhammad).

فَإِنِ اسْتَكْبَرُوا فَالَّذِينَ عِنْدَ رَبِّكَ يُسَبِّحُونَ لَهُ بِاللَّيْلِ وَالنَّهَارِ وَهُمْ لَا يَسْأَوْنَ ۗ

وَمِنَ آيَاتِهِ أَنْ تَرَى الْأَرْضَ خَاشِعَةً فَإِذَا أَنْزَلْنَا عَلَيْهَا الْمَاءَ اهْتَزَّتْ وَرَبَتْ وَأَنَّ الْأَنْدَادَ أَحْيَاهَا لِمَجَى الْمَوْتَىٰ إِنَّهُ عَلَىٰ كُلِّ شَيْءٍ قَدِيرٌ ۝

إِنَّ الَّذِينَ يُلْجِدُونَ فِي آيَاتِنَا لَا يَحْفَظُونَ عَلَيْهَا ۗ أَمْ كُنْ فِي الشَّرْحِ خَيْرٌ أَمْ كُنْ يَاقِينَ ۗ إِنَّمَا يَوْمَ الْقِيَامَةِ إِعْمَلُوا مَا شِئْتُمْ إِنَّهُ بِمَا تَعْمَلُونَ بَصِيرٌ ۝

إِنَّ الَّذِينَ كَفَرُوا بِالذِّكْرِ لَمَّا جَاءَهُمْ ۗ وَإِنَّهُ لَكِتَابٌ عَزِيزٌ ۝

لَا يَأْتِيهِ الْبَاطِلُ مِنْ بَيْنِ يَدَيْهِ وَلَا مِنْ خَلْفِهِ ۗ تَنْزِيلٌ مِنْ حَكِيمٍ حَبِيبٍ ۝

مَا يُقَالُ لَكَ إِلَّا مَا قَدَّ قِيلَ لِلرُّسُلِ مِنْ قَبْلِكَ ۗ إِنَّ رَبَّكَ لَذُو مَغْفِرَةٍ وَذُو عِقَابٍ أَلِيمٍ ۝

وَلَوْ جَعَلْنَاهُ قُرْآنًا عَجَبِيًّا لَقَالُوا لَوْلَا فُصِّلَتْ آيَاتُهُ أَءَعْجَبِيٌّ وَعَرَبِيٌّ ۗ قُلْ هُوَ لِلَّذِينَ آمَنُوا هُدًى وَشِفَاءٌ ۗ وَالَّذِينَ لَا يُؤْمِنُونَ فِي آذَانِهِمْ وَقُفُوفَهُمْ وَعَلَيْهِمْ عَذَابٌ أُولَئِكَ يُنَادُونَ مِنْ مَكَانٍ بَعِيدٍ ۝

وَلَقَدْ آتَيْنَا مُوسَى الْكِتَابَ فَاحْتَلَفَ فِيهِ ۗ وَلَوْلَا كَلِمَةٌ سَبَقَتْ مِنْ رَبِّكَ لَفُضِيَ بَيْنَهُمْ ۗ وَاللَّهُمَّ لَعْنَىٰ شَيْئِكُمْ مِنْهُ مُرِيبٌ ۝

42. Tumeyasema haya na kuyatolea mifano yake mara chungu nzima.

43. Tumesema haya katika Aya ya 3 ya *Suratul Muumin*.

44. Hawa — kama inavyosemwa mara nyingi — wanatafuta visingizio vya uwongo tu.

46. Anayefanya mema anajifanyia (mwenyewe) nafsi yake, na mwenye kutenda ubaya ni juu (ya nafsi) yake (vile vile); na Mola wako si dhalimu (hata kidogo) kwa waja (wake).

47. Ujuzi wa kujua Kiama unarudishwa Kwake (tu Mwenyezi Mungu). Na matunda hayatoki katika mafumba yake, (vifuniko vyake), wala mwanamke hachukui mimba wala hazai ila kwa ujuzi wake. Na siku atakayowaita (Mwenyezi Mungu akawaambia): "Wako wapi washirika wangu?" Hapo watasema (hao washirikina): "Twakiri kwako ya kuwa hakuna miongoni wetu anayeshuhudia (kuwa Wewe una mshirika)."

48. Na wale waliokuwa wakiwaabudu zamani, sasa wamewapotea, na wameyakinisha ya kuwa hawana pa kukimbilia.

49. Mwanaadamu hachoki kuomba dua za kheri, (na Mwenyezi Mungu anampa, na shukrani hana); na inapompata shari, mara hukata tamaa na kuwa na bila tumainio lolote.

50. Na kama tukimuonjesha rehema yetu baada ya dhara iliyomgusa, mara husema: "Haya nayastahiki mimi (mwenyewe; hapana haja ya shukrani), wala sidhani ya kwamba Kiama kitatokea; na kama nikirudishwa kwa Mola wangu (haidhuru); bila shaka nina mema (yangu) kwake." Basi tutawajulisha wale waliokufuru hayo waliyoyatenda na tutawaonjesha adhabu ngumu.

51. Na tunapomneemesha mwanaadamu, hugeuka na kujitenga upande, (hana haja ya kutuabudu); na inapomgusa shari, mara hugeuka akawa ana madua marefu marefu.

52. Sema: "Mwaonaje! Ikiwa (maneno haya) yametoka kwa Mwenyezi Mungu, kisha nyinyi mkayakanusha (si mumepotea hivyo kwani), ni nani aliyepotea zaidi kuliko yule aliye katika upinzani wa mbali (kabisa na haki)?"

53. Tutawaonyesha (ukweli wa) maneno yetu haya katika nchi za mbali na katika nafsi zao wenyewe mpaka iwabainikie kwamba haya ni kweli. Je! Haikutoshi kwa Mola wako kuwa Yeye ni mjuzi wa kila kitu?

54. Tahadharini! Wamo katika shaka katika kukutana na Mola wao! Hakika Yeye (Mola wao) amekizunguka, (anakijua vyema) kila kitu.

مَنْ عَمِلَ صَالِحًا فَلِنَفْسِهِ وَمَنْ أَسَاءَ فَعَلَيْهَا
وَمَا رَبُّكَ بِظَلَّامٍ لِلْعَبِيدِ ﴿٥٠﴾

إِلَيْهِ يُرَدُّ عِلْمُ السَّاعَةِ وَمَا تَحْتُمِرُونَ مِنْ ثَمَرَاتٍ
مِمَّنْ أَكْتَامُهَا وَمَا تَحْمِلُونَ مِنْ أُنْثَىٰ وَلَا تَضْمُونَ إِلَّا
بِعِلْمِهِ ۚ وَيَوْمَ يُنَادِيهِمْ إِيَّانَ شُرَكَاءِئِي ۖ قَالُوا
أَذْنَابُكُم مَّا مَاتْنَا مِنْ شَهِيدٍ ﴿٥١﴾

الظلمة العاصية والخبيرون (٥٠)

وَصَلَّىٰ عَنْهُمْ مِمَّا كَانُوا يَدْعُونَ مِنْ قَبْلُ
وَوَطَّأُوا مَا لَهُمْ مِنْ مَّوْجِيعٍ ﴿٥٢﴾

لَا يَسْتَمِعُ إِلَّا لِنَاسٍ مِنْ دُعَاءِ الْخَيْرِينَ وَإِنَّ لَكُمْ فِي
الشَّرِّ لَلْيُسْرَىٰ قَنُوطٌ ﴿٥٣﴾

وَلَيْنَ أَذَقْنَاهُ رَحْمَةً مِنَّا مِنْ بَعْدِ ضَرَاءٍ مَسَّةٍ
لَيَقُولَنَّ هَذَا لِي وَمِمَّا أَظُنُّ السَّاعَةَ قَائِمَةً ۖ
وَلَيْنَ سُجِّعْتُ إِلَىٰ رَبِّي إِنْ لِي عِنْدَهُ لِلْحَنَنِ
فَلَنُكَلِّبَنَّ الَّذِينَ كَفَرُوا فِيهَا عَمَلُوا ۚ وَكَذَلِكَ نَقُفُّهُمْ
مِّنْ عَذَابٍ غَلِيظٍ ﴿٥٤﴾

وَإِذَا أَعْمَنَّا عَلَىٰ الْإِنْسَانَ آخِرَ صَبْرٍ وَأَنَا بِنَجَابِنِهِ
وَإِذَا مَسَّهُ الشَّرُّ فَذُوٌّ دُعَاءٍ عَرِيضٍ ﴿٥٥﴾

قُلْ أَرَأَيْتُمْ إِنْ كَانَ مِنْ عِنْدِ اللَّهِ ثُمَّ
كَفَرْتُمْ بِهِ مِنْ أَضَلُّ مِمَّنْ هُوَ فِي شِقَاقِ
بَعِيدٍ ﴿٥٦﴾

سَأْرِيهِمْ ابْنَتَا فِي الْأَفَاقِ وَفِي أَنْفُسِهِمْ حَتَّىٰ
يَتَّبِعِينَ لَهُمُ اللَّهُ الْحَقُّ ۚ أَوَلَمْ يَكْفِ بِرَبِّكَ أَنَّ اللَّهَ
عَلَىٰ كُلِّ شَيْءٍ شَهِيدٌ ﴿٥٧﴾

أَلَا إِنَّهُمْ فِي مَرِيضَةٍ مِّنْ لِّقَاءِ رَبِّهِمْ ۚ أَلَا إِنَّهُ
يَكُلُّ شَيْءًا مَّحِيطٌ ﴿٥٨﴾

٥٨

53. Tumebainisha mara nyingi baadhi ya hayo yaliyosemwa katika Qurani ambayo hayakuwa yakidhaniwa kuwa yataitakidiwa seuze kuonekana kutokea. Sasa yametokea na ulmwengu mzima yameonekana.